

FaithLife Ministries

“Kuwaanda viongozi wa kanisa duniani”

Usimamizi Kwa Viongozi Wa Kanisa

Mwongozo wa mafunzo

Toleo la # kwanza

“Kuwasaidia viongozi wa kanisa
Kusimamia huduma”

@2010, 2006, 2002 by Barry Voss
Haki zote zimehifadhiwa na
Faithlife Ministries, Inc
www.faithlifeministries.net
PHONE: (770) 492 – 4903
Email: BarryVoss@comcast.net

Utangulizi

Jarida hili limeandaliwa kuwasaidia wachungaji wanaofanya kazi makanisani, na viongozi wa huduma waliyo katika mamlaka ya usimamizi na uongazi katika ofisi za huduma. Shule nyingi za Biblia na Seminari huwafunza wachungaji na viongozi wa huduma kuhubiri, kufunza na kufunza uinjilisti, lakini mafundisho yao hayawafunzi jinsi ya kusimamia huduma zao. Kwa kuwa wachungaji wengi na viongozi ni lazima waongoze watu kusimamia rasilimali na kusimamia kanisa, mafundisho haya ni muhimu kwa kazi ambayo wameitiwa kufanya kwenye huduma zao.

Mwandishi wa kitabu hiki amekuwa akifundisha viongozi wa huduma kuanzia mwaka wa 1996. Jarida hili lilibuniwa alipofanya kazi na wachungaji katika nchi mbali mbali za ulimwengu na kuona vile viongozi hao hawakuwa na usimamizi bora wa rasilimali. Na ilikuwa vigumu kupata marejeleo ya kufunza. Kwa hivyo, kwa kuwa wachungaji wengi na viongozi wa huduma wa mataifa ambayo hayajaendelea, hawana elimu ya kutosha wa usimamizi wa huduma zao, Faithlife Ministries imeandaa jarida hili kuziba pengo hilo.”

Mafundisho ya jarida hili, yameandaliwa kwa njia ya kimsingi kabisa, ili iwe rahisi kuelewa na kufunza kwa njia ya Biblia na ya ukiristo. Vifaa hivi vinapotumiwa kwa njia nzuri na kumtegemea Roho Mtakatifu matokeo yake yatakuwa makubwa na yatazaa matunda kwa ufalme wa Mungu.

**@ 2010, 2006, 2002 na Barry Voss, Faithlife Ministry, Inc
Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya jarida hili ambayo hutolewa, kuwekwa katika tarakilishi, na kurekodiwa katika mashini zozote zile bila idhini ya mwandishi, ila tu kuruhusiwa na jumua ya Marekani (Copy Right Law).**

Kuhusu FaithLife Ministries

Faith life Ministries ilianzishwa mnamo mwaka wa Januari 2001 na Barry Voss na Kim Star Voss ili kutoa mafunzo ya huduma ya Kikristo na rasilimali kwa viongozi wake ulimwenguni. Mwito na shauku ya kuona watu wakifanyika wakristo kuwakamilisha watakatifu na kuwapa mafunzo watu wa Mungu, Haswa katika maeneo ambayo mafunzo ya aina hii hayapatikani kwa urahisi au gharama yake ni ya juu. Wamekuwa wakiwafundisha wachungaji, viongozi wa vijana, watoto na hata vikundi vya watu wazima katika mataifa mbali mbali msisitizo wao ukiwa ni kukuza uongozi wa huduma na ujuzi wake. Kando na kufanya **warsha** na kongamano wanahusika katika kuandaa mafundisho na kuhimiza waumini kuishi maisha ya imani.

Hapo mwanzo Kim alikuwa mwalimu wa kufundisha watoto katika kanisa la Shepherd Church kule Alpharetta, GA ambapo aliwahudumia watoto na watu wazima kwa zaidi ya miaka tano. Pia amewahi kufanya kazi zaidi ya miaka kumi na mitano kama mkurugenzi kwenye kampuni inayohusika na mitambo ya tarakilishi kando na mashirika mengine makubwa. Barry amejiriwa katika huduma hii ya Faith Life Ministries ana takribani miaka ishirini katika usimamizi wa biashara. Anahusika katika huduma ya ibada na kikundi cha wanaume. Kim na Barry wameoana kwa miaka thelathini na mitano na wana watoto wawili wakubwa.

Shukrani

Ningependa kutoa shukrani kwanza kabisa kwa Mungu kwa kuwezesha mradi huu kufaulu, na kwa kutupa maono ya kutengeneza kitabu hiki cha kufunza. Pia tungependa kuwashukuru Ken Jacques, Daryl Hoh, Doming Orprecio, Ayub Khayo na David Quispirroca kwa mchango wao kwenye mafunzo haya.

Usimamizi kwa viongozi wa kanisa

Toleo la kwanza

Yaliyomo

Sehemu ya kwanza - Usimamizi wa Huduma

- Sura ya kwanza - Uongozi wa huduma
- Sura ya pili - Kuwa kiongozi wa Biblia
- Sura ya tatu - Mitindo ya uongozi
- Sura ya nne - Kuendeleza viongozi

Sehemu ya pili - Usimamizi wa watu

- Sura ya tano - Karama za Kiroho
- Sura ya sita - Kusimamia watu
- Sura ya saba - Kutatua migogoro

Sehemu ya tatu - Usimamizi wa Rasimali

- Sura ya Tisa - Mipango ya Kimkakati
- Sura ya kumi - Kusimamia fedha
- Sura ya kumi na moja - Kusimamia wakati
- Sura ya kumi na mbili - Kusimamia habari

Sehemu Ya Kwanza

USIMAMIZI WA HUDUMA



Sura ya Kwanza

USIMAMIZIWA HUDUMA

*“Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo: si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi.”
1 Petero 5:2-4”*

Uongozi bora ni wa muhimu kwa kila kiongozi kanisani. Bila hili, viongozi wengi huona vigumu kuendeleza huduma na pia kuwahusisha watu kanisani. Kimsingi uongozi ni uweza wa mtu kuwapa watu wengine motisha ili kutimiza lengo. Uongozi pia unahusisha maono na mpango, kuwakua watu na kutimiza lengo. Katika sura hii tutaangalia vipengele vitano vya usimamizi bora wa huduma.

Swali: Je sifa zipi zinamfanya mtu kuwa kiongozi?

Jibu: Wafuasi!

***Ikiwa hakuna mtu anayekufuata, wewe sio kiongozi**

Hatua tano za muhimu za uongozi (usimamizi) bora wa huduma

I. Viongozi hutumia ushawishi wao, sio mamlaka walio navyo

Yohana 10:2-4

“Aingiaye mlangoni ni mchungaji wa kondoo. Bawabu humfungulia huyo, na kondoo humsikia sauti yake; naye huwaita kondoo wake kwa majina yao, na huwapeleka nje”

❖ Uongozi ni ushawishi

- 1) Yakupasa kuwapa watu motisha kwa kuwahamashisha
- 2) Utakuwa na ushawishi kwa kuaminika na kuwaheshimu wenzako
- 3) Uongozi ni uweza wa kushawishi na kuwaleta wengine kufuata maamuzi yako kwa hiari

❖ **Mamlaka** ni nguvu au uweza

1) Kulingana na kamusi, mamlaka ni:

“Ni uweza wa kushawishi ao kuelekeza wazo, maoni au tabia”

2) Mamlaka yamepeanwa na Mungu kwako

“Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isioyotoka kwa Mungu.” – Warumi 13:1

3) Mamlaka huja kwa yale uliyotekeleza awali sio yale unayotenda sasa

4) Mamlaka ni uwezo wa **kutekeleza** maamuzi yako

- Tutatumiaje mamlaka yetu?
 - Kwa kufundisha

“Lakini wewe nena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima. Nena maneno hayo, onya na kukaripia kwa mamlaka yote.” - Tito 2:1,15

- Kwa kutumika

“Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo – IPetro 5:2

**Nivyema wakati wote kuongoza ukitumia ushawishi wako badala ya mamlaka uliyo nayo.

- Ukitumia ushawishi wako watu watataka kukufuata
- Ukitumia mamlaka yako utawalazimu watu kukufuata
 - Utawapoteza watu kwenye huduma yako
 - Kutakuwepo na upinzani

II. **Viongozi wana maono**

- ***Mithali 29:18 “pasipo maono watu hukosa kujizuia.”***

1. Kiongozi hufahamu anakoelekea

2. Bila maono kanisa halina mwelekeo

- Maono huleta mwelekeo
- Hueleza kwa kina makusudi na lengo la kanisa

3. **Maono huelezea lengo na mathumuni ya huduma**

- Mathumuni yake na lengo inalokusudia kutimiza
- Inachotaka kuwa au kufanya

- **Mifano ya maono**

1. Kulijenga jengo jipya la kanisa kwa muda wa miezi kumi na miwili
2. Kuanzisha kituo cha kuwalisha maskini katika jumuiya
3. Kuanzisha shule yenye maadili ya kikiristo kwenye jumuiya
4. Kuwafikia watu elfu kumi na injili

4. Maono yanalisadia kanisa kutimiza lengo lake

- Maono aliyopeana Mungu sio jambo rahisi la kutekeleza kwa uwezo wetu wenyewe *Yohana 15:5 – “Pasipo mimi ninyi hamwezi lolote.”*
- Ni muhimu kwa kanisa kutafuta mwongozo wa Mungu *Mathayo 19:26 –“kwa Wanadamu hilo halowekani bali kwa Mungu yote yanawezekana.”*

5. Maono hushirukisha hulihamasisha kanisa na kulitia nguvu

- Washirika wanaposhirikishwa kwenye maono, kuna uwezakano mkubwa wao kuchangia zaidi.
- Maono huwapa watu kitu cha kutegemea kufanya kazi nacho
- Maono huwasaidia watu wajihisi kuwa wao ni sehemu kubwa ya kutegemewa

**** Maono ni tofauti na taarifa ya tume**

Taarifa huelezea unayofanya, sio unakokwenda.

Jinsi ya kuendeleza Maono

- Hatua 1** Omba Mungu akuongoze na akupe ufunuo
- Muombe Mungu akuonyeshe jinsi anavyoweza kukutumia
 - Muulize Mungu anataka umfanyie nini
- Hatua 2** Panua mawazo
- Usije ukajiwekea mipaka kutokana na ulicho nacho
 - Mruhusu Mungu akukupatiye uachohitaji
- Hatua 3** Wahusisha viongozi wengine katika maendeleo
- Hatua 4** Andika maono ukizingatia njia zingine
- Uwe na muda wa kuomba na kutafakari
 - Uliza wengine ili wakupe ushauri
- Hatua 5** Omba na uchague maono unayohisi Mungu anakuitia
- Hatua 6** Zungumza kuhusu maono (Ongea kuhusu maono)
- Kujenga hamasa na kuwahusisha wafuasi wako
 - Kutoa lengo na mwelekeo bora kwa wafuasi wako

3. **Viongozi wana mpango**

Methali 16:3

“Mkabidhi Bwana kazi zako na mawazo yako yatathibitika”

- a. Kiongozi huwa na mpango jinsi ya kutimiza maono
 - Bila mpango huenda usitimize maono
 - Maono hukuelekeza jinsi ya kupanga mikakati na raslimali
 - Kiongozi hawezi kupanga bila ya kuwa na maono
- b. Kiongozi husimamia raslimali alizopewa na Mungu
 - Mungu huwapa viongozi rasilimali wazitumie
 - Mungu anatarajia raslimali zitumiwe vyema
 - Mungu anatarajia matunda, matokeo kwa raslimali alizopeana
- c. Kazi ya kiongozi ni kupanga kazi na mipango mikakati
 - Ni lazima kiongozi aboreshe mpango wake
 - Mpango mzuri humsaidia kiongozi kufanya maamuzi bora
 - Mpangilio mwema huepusha hali yakutumia vibaya raslimali anazo tupa Mungu

4. **Viongozi huwaendeleza watu**

Luka 9:1-2

“Akawaita wale thenashara akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi. Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu na kupoza wagonjwa.”

- a. Viongozi huwafanya watu kuwa wanafunzi kwanza – *(Mathayo 28:19-20)*
 - Kufundisha na kulihubiri neno
 - Wafunze kutii
- b. Viongozi huwapa wengine mafunzo na vifaa kwa ajili ya huduma
 - Viongozi huwafundisha kujua na kutumia vipawa vya kila mmoja
 - Huwachochea watu kuhusika kwenye huduma
- c. Viongozi huteua na kuimarisha viongozi wengine
 - Jinsi ya kukuza huduma zao
 - Kuendeleza huduma
 - Viongozi wanavyoongezeka ndivyo nafasi ya ufanisi pia

5. Viongozihulenga matokeo

Warumi 14:12

“Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.”

- a. Viongozi huzingatia kukamilisha lengo na kupata matokeo
 - Kiongozi huzingatia daima akilini mwake maono
 - Kiongozi hupima ufanisi kwa matokeo yanayopatikana
- b. Viongozi hulenga maeneo yaliyo na matokeo makubwa ya uwekezaji wao
 - Kiongozi huelekeza raslimali zake kwa eneo liletalo matunda zaidi
 - Kiongozi hujitenga na huduma zisizozaa matunda
- c. Viongozi huelewa kwamba shughuli nyingi hazimaanishi mafanikio yatakuwepo
 - Kiongozi hupima umuhimu wa huduma tofauti kwa matokeo yake
 - Kiongozi hudhamini shughuli kulingana na maono yake

Luka 10:38-42

“Ikawa katika kuenenda kwao aliingia katika kijiji kimoja: mwanamke mmoja jina lake Martha akamkaribisha nyumbani kwake. Naye alikuwa naaitwaye Mariamu, aliyekei miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake. Lakini Martha alikuwa akihangaika kwa utumishi mwingi; akamwendea, akasema, “Bwana, huoni vibaya hivyo ndugu yangu alivyoniacha nitumike pekee yangu? Basi mwambie anisaidie.” Bwana akajibu akamwambia, “Martha Martha unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; lakini kinatakiwa kitu kimoja tu; na Mariamu amelichagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa”

(Andiko hili linatuonyesha ya kwamba Martha alijihusisha na shughuli lakini Mariamu alikazia matokeo.)

Dira na maono

1. Andika tamko la dira (Je Mungu anakuita umfanyie nini?)

2. Andika tamko la maono (Je, Mungu ametupa lengo lipi la huduma kutimiza?)

** Ujumbe wa tamko la maono lazima uwe na kipimo cha kukamilishwa

Sura ya Pili

KUWA KIONGOZI WA BIBILIA

Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa nje kamatawi na kunyauka watu huyakusanya, na kuyatupa motoni yakateketea. Ninyi mkikaa ndani yangu namaneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi, mtatendewa kwavile mzavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.

Yohana 15:5-8

Tunapowaongoza wengine, kuzifuata kanuni za Bibilia ndilo neno la umuhimu ambalo kiongozi anweza kulitamani sababu hayo ndiyo Yesu alikuja kutufundisha. Hata kama yanaonekana kwamba siyo ya muhimu kwetu, tukizifuata njia za Mungu badala ya njia zetu wenyewe tutakuwa na huduma yenye matokeo bora zaidi. Tunaweza kuwa na uwezo mkubwa wa uongozi lakini kama msingi wake sio katika neno la Mungu basi kuna uwezekano wa kuwawaongoza wafuasi wetu kwa njia isiyofaa. Katika sura hii tutatazama sifa kumi za kibiblia za viongozi na changamoto wanazokabiliana nazo viongozi wa leo

I. Utangulizi

Je lengo la kiongozi wa Ki-Kristo ni lipi?

Sio kuwa na wahudhuriaji wengi au kushirikisha

Ni..... kuona Kristo akiumbika ndani ya wengine

*“Vitoto vyangu ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu”
(Wagalatia 4:19)*

Tofauti ya kiongozi wa ki-kristo ni ipi na viongozi wengine?

Yeye hujua kuwa – **“Pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote” (Yohana 15:5)**

Sifa za kiongozi: kiongozi bora hudhihirisha sifa hizi kumi:

1. Kiongozi bora ni mwenye maono

“pasipo maono, watu huacha kujizuia” Mithali 29:18

- Yakupasa kuwa na lengo
- Wahitaji kuyaelezea kwa njia ambayo watu wengine wataweza kushiriki kwenye maono.

Mfano: Musa alipokea maono kutoka kwa Mungu kupitia kichaka kilichowaka moto.
(Kutoka 3)

2. Kiongozi bora lazima awe na..... **ujumbe wenye nia ya kazi** .
“Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake.”- Mathayo 9:37 – 38.

- Ulenge kuwafikia wasioamini.
- Jihusisheni na uongozi wa wanafunzi wengine ambao wahitaji mchungaji.

Mfano: **Paulo** (alifanya safari nyingi za kimishonari – Matendo)

3. Kiongozi bora lazima awe na..... **shauku**
“lazima sasa timizeni kule kutenda nako ili kama mlivyokuwa tayari kutaka vivyo hivyo mkawe tayari na kutimiza, kwa kadiri ya mlivyo navyo”2wakorintho 8:11
- Lazima uijali zaidi huduma yako.
 - Lazima ujitolee ili ufanikiwe (shauku = kujitolea)

Mfano: **Stephano** (alikuwa amejitolea katika huduma – Matendo 7)

4. Kiongozi bora lazima ... **aongozwe na Roho**
“Lazima mtapokea nguvu, akiisha kuwatilia juu yenu Roho Mtakaatifu nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wan nchi” Matendo 1:8
- Mruhusu Roho Mtakatifu akuongoze
 - Uwe na mawasiliano kamili na chanzo chako cha nguvu – Roho Mtakatifu.

Mfano: **Daniel** (hangeikana imani yake – Daniel – 6)

5. Kiongozi bora lazima awe... **Mtumishi**
“Lakini haikuwa hivyo kwenu, bali mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu kama vile mwana wa adamu asivyokuja kutumikiwa bali kutumika na kutoa nafsi yake iwe fidia kwa wengi.”Mathayo 20:26 - 28
- Kiongozi ameitwa kuwatumikia wafuasi wake wala si kutumikiwa.
 - Kiongozi bora huwasaidia wafuasi wake kukua na kufanikiwa.

Mfano: **Yesu** (akiwaosha wanafunzi wake miguu – Yohana 13)

6. Kiongozi bora lazima awe na..... **Umakini**
“Ndugu sijidhani nafsi yangu kwamba mimekwisha kushika, ila natenda neno moja tu nikiyasahu yaliyo nyuma nikiyachuchumilia yaliyo mbele nakaza mwendo.....mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo YESU.” Wafilipi 3”13 – 14
- Usijiingize kwa maswala ambayo hayahusiani na maono na dira yako.
 - Isimruhusu Shetani akupotoshe.

Mfano: **Nehemia** (alilenga katika kuzijenga kuta za Yerusalemu – Nehemia 6)

7. Kiongozi bora lazima awe na.....**ujasiri**

“Musa akamuita Yoshua akamwambia machoni pa Israel wote uwe hodari na moyo wa ushuja maana utakwenda pamoja na watu hawa hata nchi Bwana aliwaapia baba zao, ya kwamba atawapa nawe atawarithisha naye Bwana ndiye atakaye tangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha, usiogope wala usifadhaike”
Kambukumbu la Torati 31:7- 8

- Kiongozi huchukua hatua ya imani.
- Kiongozi huwa tayari kuhatarisha ili kupokea ufanisi mkubwa.
- Mungu atakukamilisha na kukupa nguvu.

Mfano: **Daudi** (vita vyake na Goliathi – 1 Samuel 17)

8. Kiongozi bora anahitajika kuwa mtu mwenye..... **Kutumaini.**

“Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe”
Mithali 3:5

- Kiongozi humtumaini Mungu ambaye ni mwaminifu na wa kweli.
- Kiongozi humtumaini Mungu hata hali inapoonekana tofauti

Mfano: **Abrahamu** (kumtoa Isaka kama thabihu Mwanzo 22).

9. Kiongozi bora lazima awe...**amejiandaa**

- Maandalizi yanaleta utayari wa kujitolea na kupanga.
 - Ufanisi ni kuhusishwa ni 1% na.... kujiandaa asilima tisini na tisa (99%).
- « Lihuburi neno uwe tayari, wakati ukufaa na wakati usiokufaa karipia, kemea na kuonya kwa utulivu wote na mafundisho »* **2 Timotheo 4:2**

Mfano: **Yusufu** (aliandaa kukabiliana na njaa – Mwanzo 41).

10. Kiongozi bora lazima azitumie fursa zilizoko..... **Nyemelezi**

“Tena tusichoke katika kutenda mema, maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho kwa hivyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema, na hasa jamaa ya waaminio” **Wagalatia 6:9-10.**

- Furahia siku (tumia nafasi ambazo Mungu anakupa leo).
- Uwe makini kuzitambua fursa hizo zinapojitokeza.

Mfano: **Esta** (aliwaokoa watu wake kutoangamizwa Esta 4).

II. Changamoto za Uongozi

“Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa”
2Timotheo 3:12.

Uongozi una changamoto zake.

- A. Ukweli ni kwamba sherti awepo kiongozi mmoja kwenye usukani wa juu
 - 1. Kuwa na hekima
 - 2. Kuwa haki
 - 3. Fanya maamuzi

- B. Sio kila mtu atakubaliana nawe kila wakati.
 - 1. Tarajia watu kupinga maamuzi yako.
 - 2. Watu wana mitazamo tofauti kuhusu maswala.
 - 3. Uwe tayari kuyatetea maamuzi yako kimaandiko wala sio kwa kutumia hisia zako.

- C. Ni rahisi kushinda pigano lakini ukapoteza vita.
 - 1. Usije ukapoteza maono yako ya mda mrefu unapotazama malengo ya muda mfupi.
 - 2. Usilegeze uliyoamua kutekeleza.
 - 3. Kuwa rahisi, bila kuachana na kanuni yako kamwe

ZOEZI

KUJITATHIMINI KAMA KIONGOZI

Maelezo: Jipe alama kwa kila sifa kulingana na maneno yafuatayo

1 = Mara chache 2= Wakati mwingine 3= Mara kwa mara 4= Kawaida 5= Daima

Sifa	Alama
I. Mwenye maono	_____
II. Ujumbe wenye nia ya kazi	_____
III. Shauku	_____
IV. Kuongozwa na Roho	_____
V. Mtumishi	_____
VI. Mwenye lengo na dira	_____
VII. Ujasiri	_____
VIII. Kuamini	_____
IX. Kujiandaa	_____
X. Kutumia fursa	_____
Jumla	_____

Jumla ya Maana yake

- 40+ Unadhihirisha ujuzi mkubwa wa uongozi. Mungu anaweza kukutumia.
- 30 – 39 Unaweza kuwa kiongozi lakini bado una nafasi ya kuboresha.
- 20 – 29 Mara kwa mara umedhihirisha uongozi una maeneo kadhaa ya kujiendeleza.
- 10 – 19 Mbinu zako za uongozi ni dhaifu. Mafunzo mwafaka na kuboreshwa yanahitajika.
- 0 – 9 Haujadhihirisha uweza wa uongozi. Tafuta mafunzo zaidi au kazi nyingine.

Sura Ya Tatu

MITINDO YA UONGOZI

“Naye alitoa wengine kuwa Mitume: na wengine kuwa wanabii, na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungani na walimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke; hata mwili wa Kristo ujengwe”

Waefeso 4:11-12.

Mungu amemuita kila kiongozi kulingana na uwezo alio nao, ili kuwaanda watu wa Mungu kwa kazi za huduma na kuujenga mwili wa Kristo. Kila mmoja wetu ni tofauti, kama viongozi, kimsingi tunaongoza, kusimamia na kuendesha kulingana na utu wetu, karama na uzoefu. Katika mazingira tofauti tofauti mtindo tunayotumia unaweza kuwa na matokeo bora kwa wamoja na kwa wengine unaweza ukawa na matokeo mabaya. Kuelewa mtindo wetu au mitindo ya wenzetu ya uongozi itatusaidia kwa njia kubwa kuwa na ufanisi zaidi katika hali ya kutumia uwezo wetu wa uongozi katika hali tofauti. Katika sura hii tutatazama mitindo minne ya uongozi na jinsi inavyoweza kutumiwa kwa ubora zaidi.

I. Mitindo ya Uongozi ni ipi?

- Kuna aina nne za mitindo ya uongozi, kulingana na **George Barna** katika kitabu chake **“A fish Out of water”** (intergrity publishers 2002).

1. Kiongozi wa kuelekeza.

- Kiongozi huyu kimsingi ni mtu mwenye maono
- Kiongozi huyu huzingatia matokeo wala sio njia itakayo tumiwa kusababisha matokeo haya.

2. Kiongozi wa Kimkakati

- Kiongozi huyu hupenda kuchambua habari na kuchunguza maswala kwa kina.
- Kiongozi huyu hupenda kuendeleza na kuwa na mipango inayohusiana na maono.

3. Kiongozi mwenye kujenga kundi

- Kiongozi huyu anajali sana mahusiano ya watu kuliko kutimiza kazi tu.
- Kiongozi huyu huwaleta watu pamoja ili kutimiza maono.

4. Kiongozi wa Uendeshaji

- Kiongozi huyu huunda mifumo ili kuhakikisha maono yametekelezwa.
- Kiongozi huyu hupenda kujenga mfumo na kufuatilia matokeo

II. Kuamua mtindo wa Uongozi wako

Mtindo Wako wa Uongozi ni Upi?

Zifuatazo ni semi zinazo husiana na tabia za uongozi. Soma kila moja kwa makini na kisha tambua mtindo wako wa uongozi, tumia maneno yafuatayo, yatakusadia kujua mtindo wako wa uongozi. Kwa matokeo thabiti kwa uaminifu.

Kamwe 0	Mara Chache 1	Wakati mwingine 2	Mara nyingi 3	Kawaida 4	Huwa daima 5
------------	------------------	----------------------	------------------	--------------	-----------------

1. _____ Mimi huwatia moyo walio kwenye kikundi changu kutekeleza maamuzi na mapendekezo yao.
2. _____ Hakuna lililo la muhimu kwangu kuliko kufanikisha lengo.
3. _____ Kuwaheshimu na kuwathamini watu ni jambo ninalolipa kipaumbele cha juu.
4. _____ Mimi hufuatilia ratiba kwa makini ili kuhakikisha kazi au mradi umekamilika kwa wakati.
5. _____ Hufurahia kuwapa watu mafunzo mapya ya kazi na taratibu.
6. _____ Jukumu linavyokuwa na changamoto zaidi ndivyo linavyo nisisimua.
7. _____ Huwatia wengine moyo kuwa wabunifu katika kazi zao.
8. _____ Ninaposimamia mradi mgumu nazingatia kilajambo dogo na kubwa.
9. _____ Hufurahia kusoma makala, vitabu na majarida yanayohusu mafunzo yaviongozi na saikolojia nikiyatekeleza niliyoyasoma.
10. _____ Ninaweza kutekeleza majukumu ambayo sio mepesi kwa wakati mmoja.
11. _____ Ninaporekebisha makosa ya wengine, huhofia kuhatarisha uhusiano
12. _____ Hutumia muda wangu inipasavyo.
13. _____ Hufurahia kueleza vipengele tata na vya maelezo ya miradi ya kazi ngumu kwa watu ninaongoza.
14. _____ Kuigawanya miradi mikubwa katika sehemu ndongo ndogo inayosimamiwa vyema ni asili yangu ya pili.
15. _____ Nathamini zaidi kujenga kikundi thabiti, kujenga uhusiano/ umoja katika kundi.
16. _____ Hufurahia kuchambua matatizo.
17. _____ Naheshimu mipaka ya wenzangu.
18. _____ Nafurahia kusoma majarida na vitabu vinavyohusu huduma na kisha kukeleza taratibu mpiya niliyojifunza.
19. _____ Nafurahia kujenga wengine kuboresha utenda kazi wao.
20. _____ Hufurahia shughuli za maandalizi na mipango.

Sehemu ya Alama

Baada ya kumaliza kujibu maswali yaandike majibu yako katika nafasi iliyoachwa wazi:

Watu

Swali

1. _____
3. _____
5. _____
7. _____
9. _____
11. _____
13. _____
15. _____
16. _____
17. _____
19. _____

Kazi

Swali

2. _____
4. _____
6. _____
8. _____
10. _____
12. _____
14. _____
16. _____
17. _____
18. _____
20. _____

Jumla _____

(Gawa jibu kwa kumi halafu jumlisha nambili)

Jumla _____

(Gawa jibu kwa kumi halafu jumlisha na mbili)

Alama _____

Alama _____

Sehemu ya matokeo

Angalia alama zako za mwisho katika mchoro ulio hapo chini kwa kuweka alama za watu wako katika mhimili wa usawa na alama tena katika mhimili wa wima hapo chini, kisha chora laini mbili zilizo wima mpaka zikutane. Mahali ambapo laini hizo mbili zitakutana ndiyo mtindo wako wa uongozi.

1	Kujenga kikundi	Mkakati							
2									
3									
4									
5	Kuelekeza	Uendeshaji							
6									
7									
8									
9									
	1	2	3	4	5	6	7	8	9

III. Kutumia Mitindo ya Uongozi

1. Kulingana na George Barma, kila kiongozi hutumia mtindo mmoja zaidi kati ya hii minne ya uongozi. Hata hivyo viongozi wote huwa na sehemu ya kila mtindo.
2. Uzungukwe na viongozi wenye mtindo tofauti nawe.
 - Watachangia maeneo tofauti.
 - Wataona mambo kwa njia tofauti nawe.
“Pasipo mashauri makusudi huharibika; bali kwa wingi washauri huthibitika”
Methali 15:23
3. Ongoza kulingana na sifa zako bora zaidi wala sio udhaifu wako.
“basi kwa kuwa tuna karamu zilizo mbali mbali, kwa kadiri ya neema tuliyopewa: ikiwa unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani yetu; mwenye kundisha, katika kufundisha kwake mwenye kuongea, katika kuongea kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; mwenye kusimani; kwa bidii mwenye kurehemu kwa furaha.”
Warumi 12:6-8.
4. Elewa uongozi unajitokeza kulingana na hali unayokumbana nayo.
 - Mtindo wako mkuu wa uongozi huenda usiwe na mafanikio katika hali zote.
 - Tambua ni mtindo upi wa uongozi utakaokuwa na matokeo bora katika hali maalum.

Mifano:

1. Kuweka mwelekeo mpya wa huduma – **Uongozi wa kuelekeza (haswa wakati hatua inahitajika).**
 2. Imarisha mipango mipya kwa huduma yako – **Uongozi wa kimkakati (wakati uchambuzi na mpango unahitajika).**
 3. Wakati wa kusuluhisha mgogoro katika huduma yako – **Uongozi wa kujenga uhusiano (unapohitajika kufanya kazi na watu).**
 4. Kutumia teknolojia katika huduma yako – **Uongozi wa uendeshaji (wakati mifumo inapohitajika).**
- Mruhusu kiongozi mwingine kwenye kikundi aliye na mtindo mwafaka kuongoza.
 - Baki ukiwa na mamlaka makuu
 - Gawa kazi au majukumu ya miradi kwa kiongozi wa kikundi chako.
5. Kutumia mtindo usiofaa wa uongozi una madhara yake.
 - Uongozi wako unaweza kupingwa
 - Unaweza kuharibu uaminifu wako
 - Unaweza kusababisha mgogoro usiotakikana
 - Huduma inaweza kutolegea au kuathirika vibaya

Zoezi la mitindo ya Uongozi

Maelezo: Kwa kila hali katika mkono wa kushoto, andika chini mtindo mwafaka wa uongozi ambao unatakikana kutumika au unaweza kutumika. (kuelekeza, kimkakati, kujenga umoja, kuendesha) :

Hali	Mtindo wa uongozi utakotumia
1. Umepewa kompyuta kanisani na unawazia njia bora ya kuitumia.	
2. Umeanzisha huduma ya kufikia watu gerezani na hutaki kutumia rasilimali kutoka idara nyingine kanisani.	
3. Kikundi cha ibada ya sifa kimekuja kwako na malalamishi kuhusu kiongozi wa ibada ya sifa.	
4. Unajua vyema kuwa unahitaji kufikia jumuiya na injili lakini hujui njia bora ya kutekeleza jambo hili.	
5. Unataka kulihamisha kanisa lako hadi upande wa pili wa mji ambako umepata kiwanja kikubwa.	
6. Baadhi ya watu wamelalamika kuhusu ibada na wanataka ufikirie kutenda jambo tofauti.	
7. Huduma yako ya watoto imeshindwa kutimiza malengo yake na idadi ya wanaohudhuria imepungua.	
8. Watu wameanza kuhama kanisa lako na kujiunga na kanisa jirani.	
9. Kanisa lingine mjini limekuomba ruhusa kulitumia kanisa lako.	
10. Una shida ya umbea kanisani mwako.	

Sura Ya Nne

KUENDELEZAVIONGOZI

*“Bwana akamwambia Musa, mtwae Yoshua mwana wa Nuni, mtu mwenye ndani yake, ukamwekee mkono wako; kasha ukamweke mbele ya Eleazari na mbele ya macho yao.”
Hesabu 27:18-20*

Uongozi wa kanisa au wa huduma ni jukumu kubwa la kukamilisha kazi ambayo Bwana ametuitia. Mara nyingi tunadhani kuwa ukiwa kiongozi unahitajika kuhusika katika kila shughuli ya huduma ili kuongoza vyema. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba hatuwezi. Haiwezekani kuongoza kila mkutano, kusimamia kila jambo au hata kufanya kila uamuzi. Kama viongozi, ikiwa tutatimiza malengo yetu ya uongozi ipasavyo, inatupasa tutambuwe watu wengine wenye msaada na uwezo wa kushirikiana nasi. Hii inamaanisha inatupasa kuwatambua watu wengine ambao wanauwezo wa uongozi na imani ili kuwakuza waongoze, watende na kusimamia, kulingana na malengo na mamlaka. Kama jinsi Musa aliweka mikono yake juu ya Yoshua, wewe pia itakupasa kutambua viongozi wengine walio “katika Roho” na uwape tume kufanya kazi kwa niaba yako na wakiwa chini ya mamlaka yako. Katika sura hii tutatazama sifa za kiongozi, umuhimu wa kuwakuza viongozi, jinsi ya kuwatambua na kuwakuza.

I. Kiongozi ni nani?

Kulingana na Biblia, kiongozi;

1. Anajua kitambulisho ao nafasi yake katika Kristo (**2Wakorintho 5:15-21**).
 - a. Anajua ya kwamba sisi sote ni wa hudumu wa Kristo (**1Petro 2:9**).
 - b. Ametuvika nguvu zake (**Waefeso 1:18-20, 3:14-20**).
 - c. Sisi sote tunaumuhimu kwa mwili wa Kristo (**1 Wakorintho 12:27**).
2. Anaelewa kuhusu karama za kiroho
 - a. Kila mmoja amepewa karama za Kiroho (**1 Wakorintho 12:7**).
 - b. Wote tumeitwa kutumia vipawa tulivyopewa (**Waefeso 4:11-13**).
 - c. Kiongozi anawajibika kuwachochea wenzake kutumia karama zao. (**2 Timotheo 2:2**).
3. Wanafahamu kwamba kazi yao ni kuwa chumvi na nuru (**Mathayo 5:13-16**).
 - a. Lazima tuwe washawishi katika tamaduni zetu.
 - b. Sisi tu vielelezo. (**1 Wathesalonike 1:7**)
 - c. Tu wajumbe wa Kristo. (**2 Wakorintho 5:20**)
4. Amejitolea kueneza injili (**Matendo 1:8**) na kuwafanya wafuasi wa Kristo. (**Mathayo 28:19**)

II. Kwa nini ni muhimu kuendeleza viongozi?

1. Hivi ndivyo ufalme wa Mungu unavyokuwa.

- Yesu alifunza kanuni za kujumulishwa kwa huduma kupitia wanafunzi wake.
 - Yesu aliwateua viongozi ambao wangelijenga kanisa lake hapa duniani.
 - Yesu aliwapa mafunzo na akawafanya wanafunzi.
 - Aliwaambia ***“enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi”***.
Mathayo 28:19.
- Yesu hakulijenga kanisa peke yake.
“kama vile Baba alivyonituma, name nawatumeni,” John 20:21
 - Paulo alikwenda kwenye safari za kimishonari
 - Wanafunzi na wafuasi wengine walianzisha makanisa.
- Kanisa ni mwili mmoja, na kila mtu ana wajibu wake.
Sasa ninyi ni mwili wa Kristo, na kila mmoja wenu ana sehemu yake.
1 Wakorintho 12:27

2. Itazidisha huduma yako

- Inakuwezesha wewe kama kiongozi kupanua/ kusambaza huduma yako na kuongeza watu zaidi ukishirikisha viongozi ambao watahudumia wengine.
 - Huduma yako itaboresha maisha ya wengi na kuenea zaidi.
 - Huduma yako itawafikia watu wengi.
- Itakusaidia kutimiza zaidi kwa wepesi na katika muda mfupi.
 - Haiwezekani kuwa kila mahali wakati mmoja.
 - Haiwezekani kutenda mambo yote wakati mmoja.***“Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani”***
Matendo ya Mitume 6:2.
- Itakufungulia milango ambayo huenda usiione au hukuweza kuifuatilia.
 - Viongozi ulionao wana vipawa tofauti vya kushiriki
 - Viongozi ulionao wanashauku tofauti na vitu wanavyopenda havifanani.

3. Inamwezesha Roho Mtakatifu kufanya kazi ndani ya kanisa

- Roho Mtakatifu anafanya kazi kupitia watu wote na sio wachungaji tu. Sisi ni Makuhani wa Waumini.
“Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kwa mwili mmoja, kwamba tu wayahudi.”1 Wakorintho 12:13
Roho Mtakatifu huwapa nguvu waumini wote.
“Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu.”
Matendo 1:8

4. Ufanisi wa huduma au maanguko yake hutegemeana na Uongozi na Roho Mtakatifu.

- Bila ya uongozi dhabiti huduma haiwezi kufaulu.
 - Viongozi bora wanaweza kurejesha huduma ambazo haziendelei vyema.
 - Viongozi wabaya wanaweza kuharibu huduma zinazonawiri.
- Roho Mtakatifu ndiye chanzo cha nguvu zetu.
 - Sisi tu wapanzi wa mbegu tu.

***“Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji bali Mungu akuzaye.”*1 Wakorintho 3:7**

- Nguvu zetu zinatoka kwa Mungu, Roho Mtakatifu.

***“Maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.”*Yohana 15:5.**

III. Jinsi ya kutambua viongozi wengine?

1. Vigezo vya viongozi imara

a) Watu wenye maadili

“Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mme wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji ajuaye kufundisha, si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga wa kujadiliana, wala si mwenye kupenda fedha”. - 1Timotheo 3:2-3.

b) Watu wa imani

***“Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akavunja akaanguka katika hukumu ya ibilisi.”* 1Timotheo 3:6.**

“ Wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi”. 1 Timitheo 3:9

c) Watu waliojawa na Roho

***“Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho na hekima.”*Matendo 6s:3**

2. Vigezo vya viongozi ambavyo havijatajwa katika Biblia lakini hutumika

- Elimu
- Nafasi ya kiongozi kwenye jamii
- Uzoefu

****Mambo haya ni bora kuwa nayo lakini yasiwe ndio msingi wetu tunapo wachagua viongozi.**

3. Kuwachagua viongozi

- Chagua watu wenye shauku
- Wachague watu ambao wanauwezo wa kuelimishwa / kufunzwa.
- Wachague watu wanaomiliki vipawa vya kiroho vinavyohitajika

IV. Je utawakuza viongozi wengine vipi ? (tizama Mathayo 10)

Hatua ya kwanza :

Wafanye wanafunzi

- Ushauri wa kila wiki
- Watie moyo kwa manemo na matendo
- Jenga imani yao
- Waandae (kwa mafundisho ya uongozi)

Hatua ya pili :

Gawa majukumu kwao (Mathayo 10 :6-8, 16)

- Wape idara ya kuongoza au kusimamia
- Wawezeshe kutekeleza majukumu
- Jenga imani yao kibinafsi

Hatua ya tatu :

Waeleze unayowatarajia kutekeleza

- Weka malengo yaliyo wazi na kisha uwasaidie kuendeleza mpango wa uongozi
- Wape mwongozo

Hatua ya nne :

Kuwajibika (Mathayo 10 :32-33)

- Tarajia ya kuwa watatimiza lengo
- Kama kuna matatizo usiwasaidie kuyatatua ; waache wayatatue wenyewe
- Wape ushauri unao hitajika
- Wacha waje kwako wakiwa na suluhisho

Hatua ya tano :

Tathmini maendeleo yao mara kwa mara

- Kutana nao mara kwa mara kujadili maswala na matatizo yao
- Usiwaache kufanya kazi peke yao wala usiwapuuze
- Onyesha tamaa yako kwa elimu yao ili wafanikiwe

Hatua ya sita :

Wafungue katika huduma

- Wakiwa tayari, wafungue kwa huduma, wala usiwazuie
- Wape huduma waiongoze
- Watume kwa kazi ya huduma

Zoezi La Kuendeleza Viongozi

Kando na nafasi ya uongozi, andika karama za kiroho unazofikiria ni za muhimu pamoja na ujuzi au uzoefu unaofikiria ni wa muhimu kwa nafasi hiyo.

Nafasi ya huduma	Karama za kiroho	Ujuzi/uzoefu
1. Mchungaji		
2. Kiongozi wa ibada		
3. Kiongozi wa huduma ya watoto		
4. Kiongozi wa vijana		
5. Mzee wa kanisa		
6. Mwalimu		
7. Mwinjilisti		
8. Mmishonari		
9. Meneja wa fedha		
10. Kiongozi wa waombezi		

**** Rejelea kwa oradha ya karama za kiroho, ukuras 37 -38**

Sehemu ya Pili

USIMAMIZI WA WATU



Sura ya Tano

VIPAWA VYA KIROHO

Biblia inasema kuwa kila mkristo amepewa kipawa au vipawa vya kiroho kwa kujenga mwili wa Kristo. Lakini vipawa vya kiroho haswa ni nini? Je ni sawa na ujuzi na karama zetu? Je tutajuaje vipawa vya kiroho tulivyonavyo? Na tutajuaje jinsi na wapi tutavitumia? Haya ni maswali muhimu ambayo Wakristo hujiuliza wanapo taka kuelewa majukumu yao kanisani au katika mwili wa Kristo. Kama kiongozi ni muhimu kufahamu, sio kipawa chako tu mbali vipawa vya wengine pia, ili uweze kuwaelekeza katika maeneo ya huduma ambako Mungu anaweza kuwatumia zaidi. Katika sura hii tutaangalia vipawa vya kiroho haswa ni vipi, kwa nini ni muhimu, na ni vipi vitatumika kikamilifu katika huduma. Pia tutatoa tathimini ya kuwasaidia kuelewa vipawa vyenu vya kiroho.

II. Vipawa vya kiroho ni vipi?

- Vipawa vya Kiroho ni uweza ambao Roho Mtakatifu huwapa wafuasi wa Kristo kuwaandaa kwa huduma.
 1. Hivi vifaa hutolewa kwa manufaa ya wote
“Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana”¹ Wakorintho 12:7
 2. Vipawa hivi hutolewa kama Roho anavyotaka
“Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye Yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye”¹ Wakorintho 12:11
 3. Vipawa hutolewa kama vinavyohitajika
- **Vipawa vya Kiroho huwa katika vikundi vitatu**
 1. **Vipawa vya huduma** – mwito katika nafasi
 2. **Vipawa vya utendaji** – kuwahudumia wengine
 3. **Vipawa vya kikarisma**– nguvu za madhihirisho ya kiroho
- **Biblia inataja vipawa ishirini na mmoja maalum**
 1. **Huduma**
 - Mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji, mwalimu,
*“Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine Kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu”*Waefeso 4:11

2. Karama za utendaji

Huduma, kutia moyo, kukirimu, maongozi, rehema, msaada, usimamizi.

“Ikiwa huduma, tuwemo katika huduma yetu, mwenye kufundisha katika kufundisha kwake, mwenye kuonya katika kuonya kwake, mwenye kukirimu kwa moyo mweupe, mwenye kusimamia kwa bidii, mwenye kurehemu kwa furaha”.- Warumi 12:7-8

“Na Mungu ameweka wengine katika kanisa; wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu. Kisha miujiza, karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi aina za lugha. 1 Wakorintho 12:28

3. Karama za kikarisma

- Neno la hekima, neno la maarifa, kupambanua Roho, aina za lugha, tafsiri za lugha, imani, karama za kuponya, matendo ya miujiza.

“Maana mtu mmoja kwa roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye Yule. Mwingine imani katika Roho yeye Yule; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua Roho; na mwingine ni za lugha; na mwingine tafsiri za lugha.” 1 Wakorintho 12:8-10

<p>**Kuna karama nyingine ambazo zimetajwa kwenye Biblia lakini hizi ndizo zimedhirika wazi.</p>
--

II. Kwa Nini Karama Hizi Ni Muhimu?

- Kutimiza makusudi na mpango wa Mungu kwa wanadamu.
“Basi Mungu wa imani awafanye ninyi wakamilifu katika kila tendo jema.”
Waebrania 13:20-21
- Ili kuwaanda watu wa Mungu kwa kazi za huduma
“Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke”.
Waefeso 4:12
- Kuwezesha kukomaa kiroho
*“Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu hata kufika kwenye cheo cha kimo cha ukamilifu wa Kristo.”*Waefeso 4:13

Kuunganisha mwili wa Kristo

“Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo na vingo kila kimoja chake”
I Wakorintho 12:27

III. Karama Hizi za Kiroho Zinapaswa Kutumika kwa Njia Gani?

- *Kulijenga kanisa*
*“Vivyo hivyo na ninyi, kwa kuwa mnatamani sana watu wenye karama za Roho, takeni kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa”.*I Wakorintho 14:12
- Kwa kuhudumia wengine
*“Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama itumieni kwa kuhudumiana, kama wema na neema mbali mbali za Mungu”.*I Petero 4:10
- *Kumtukuza Mungu*
Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.
1 Petero 4:11
- *Kufunua tabia ya Mungu*
“Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi...” -Wagalatia 5:22-23

Mtume Paulo anatoa maonyo mawili:

- *Vipawa visipuuzwe*
*“Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako, ulivyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono na wazee.”*I Timotheo 4:14
- *Vitumike kwa utaratibu*
“Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu.”
I Wakorintho 14 :40

IV. Tathmini ya Karama za Kiroho

- **Tathmini hii ni ya kazi ipi ?**
 - Ni kifaa cha kujitambua ukitumia maswali na majibu
 - Ni kifaa cha kumsaidia mtu kutathmini karama za kiroho alizo nazo
 - Ni mwongozo wa kuwasaidia watu kanisani kuelewa majukumu yao
- Tathmini hii sio;
 - Sio mwisho wa yote kuhusu karama, karama zinaweza kubadilika
 - Usitumiwe kumzuia mtu kwenye huduma au katika utenda kazi, karama zinaweza kupeanwa na Mungu zinapo hitajika.

Jinsi ya kutambua karama za kiroho

Tazama tuvuti
<http://www.kodachrome.org/spiritgift>

Mungu amembariki kila mtu na karama za kiroho, je unafahamu vipawa ulivyopewa na Mungu ? Kama umekuwa ukijiuliza kuhusu karama ulizonazo, basi zoezi hili linaweza kukuonyesha karama hizo ni zipi.

Zoezi hili lina maswali 110 (mia moja na kumi) ambayo unajibu kwa, daima, kawaida, mara nyingi. Kuelezea jinsi unavyohisi kuhusu usemi huu.

Zoezi hili limeandaliwa na watu wala sio Mungu kwa hivyo haliwezi kuwa kamilifu. Linatakikana kutumika kama kielelezo kuhusu karama za Kiroho lakini huu sio msimamo wa mwisho. Hili ni mojawapo wa baadhi ya kifaa kinachotumiwa kueleza jinsi Mungu amekubariki ili uwe baraka kwa wengine.

Unahitaji muda wa kutosha ili kujibu semi zote la sivyo hautopokea sahihi.

Itikia kila usemi kulingana na nambari inayo ambatana na hisia inayokujia kwanza kulingana na ramana ifuatayo

Daima	5
Kawaida	4
Mara nyingi	3
Wakati mwingine	2
Mara chache	1
La	0

TUANZE

1. _____ Watu hunifuata kama kiongozi kwa urahisi
2. _____ Mimi hupenda kulitangaza neno la Mungu kwa Wakristo wenzangu
3. _____ Ni furaha kwangu kutangaza mpango wa Mungu wa wokovu kwa wasio okoka
4. _____ Hufurahia jukumu la kuwaongoza watu wengine katika maisha yao ya kiroho.
5. _____ Husisimka kuwasaidia watu kutambua ukweli katika maandiko
6. _____ Huwa na furaha ya kipekee kumwambia Mungu nyimbo za sifa nikiwa pekee au na watu wengine.
7. _____ Ni furaha ninapo wachochea watu kujitolea zaidi kwa maswala ya Kiroho.
8. _____ Wenye matatizo ya Kiroho hunijia kwa mashauri.
9. _____ Nilipokea alama bora shuleni
10. _____ mimi hupata furaha kubwa ninapofanya kazi ndogo kanisani.
11. _____ mimi hatafuta nafasi ya kuwasaidia watu katika kazi zao.
12. _____ kuna furaha kubwa kuwaongoza watu kutimiza malengo ya kikundi
13. _____ mimi hupenda kuwapanga watu kwa huduma.
14. _____ mimi hutosheka ninapotoa kiwango kikubwa cha fedha kwa kazi ya huduma.
15. _____ Mimi huhisi huruma kwa matatizo yanayowahusu wengine.

16. _____ Ni rahisi kwangu kupambanua kama mtu anasema ukweli au uwogo.
17. _____ Niko tayari kujaribu yasiyo wezekana, maana ninamtumaini Mungu.
18. _____ Nifuraha kubwa kuwapokea watu nyumbani kwangu.
19. _____ Kurekebisha vitu vilivyo haribika katika mazingira yangu si jambo gumu.
20. _____ Mimi hutambua kwa upesi mahitaji ya maombi kabla ya wengine.
21. _____ Mimi hufurahia nafasi ya kuomba na mtu aliye mgonjwa ili apokee uponyaji.
22. _____ Mimi huchangamana na watu wa jamii nyingine.
23. _____ Mimi huchukua mamlaka juu ya kikundi ninachohusiana nacho
24. _____ Mimi hupenda kushiriki neno la Mungu kuwafariji wengine.
25. _____ Ninaweza kupambanua wakati Roho Mtakatifu ameandaa mtu kumpokea Kristo.
26. _____ inasisimua ninapotoa uongozi wa kiroho kwa kusanyiko la kanisa.
27. _____ Kulifundisha darasa la Biblia ni moja ya mambo ninalofurahia kutenda au naweza kutenda kanisani.
28. _____ Mungu amenipa uweza wa kucheza chombo cha muziki, nami hufurahia jambo hili.
29. _____ Ni furaha yangu kuwatia moyo walio vunjika moyo.
30. _____ Mimi hupenda kutoa suluhisho kwa mambo yaliyo magumu katika maisha.
31. _____ Sio jambo ngumu kwangu kujifunza mambo magumu kwenye Biblia.
32. _____ Mimi hupenda kufanya kazi za kawaida kwa utukufu wa Mungu.
33. _____ Mimi hupenda kusaidia kwa kazi za dharura zinazojitokeza kanisani.
34. _____ Watu hunifuata kwa hiari tunapotekeleza swala muhimu.
35. _____ Nina furaha ninapofanya maamuzi ya muhimu.
36. _____ Mimi hupata furaha kubwa ninapotoa kiasi kikubwa cha fedha kwa huduma.
37. _____ Kuwatembelea wakongwe kwenye nyumba zao hunipa furaha kubwa.
38. _____ Hupambanua upesi kama jambo ni la kweli au la.
39. _____ Wakati mambo huonekana kama hayawezekani mimi huwa tayari kusonga mbele.
40. _____ Mimi sisumbuki wageni wanapo wasili ghafla.
41. _____ Hufurahia ninapofanya kazi ya sanaa.
42. _____ Maombi ni moja ya shuguli za kiroho ninalofurahia.
43. _____ Nimewahi kumuomba mtu aliye mgonjwa kihisia na kuona hali yake ikiboreshwa.
44. _____ Ni rahisi kwangu kufanya urafiki hata kwenye maeneo mapya.
45. _____ Sina uoga kuwaongoza watu kwenda Mungu anapotaka waenende.
46. _____ Mimi hufurahia kushiriki neno la Mungu kwa matukio ya siku kwa siku.
47. _____ Nahisi mzingo kushiriki neno injili na watu.
48. _____ Mimi hupenda kuwasaidia watu kwa matatizo yao ya kiroho.
49. _____ Watu hupata kuelewa ninapowafunza.
50. _____ Mimi hufurahia kufanya kazi na vikundi vya muziki kanisani.
51. _____ Mimi hupenda kuwatia moyo washirika wa kanisa ambao hawahusiki, kuhusika.
52. _____ Kwa kawaida watu hufuata ushauri wangu.
53. _____ Ninaweza kuelewa vifungo vingumu vya Biblia.
54. _____ mimi hutosheka ninapofanya kazi mbalimbali kanisani.
55. _____ Hupenda kufanya kazi zinazofungua wengine ili wahusike na huduma muhimu.
56. _____ Ni faida ninapowapa wengine majukumu kuliko kuyatekeleza mimi mwenyewe.
57. _____ Nafurahia kuwajibika ili malengo ya kikundi yatimie.
58. _____ Nafurahia ninapopewa nafasi ya kuchangia kifedha kwa maswala ya dharura.
59. _____ Huhisi furaha ninapo watia watu moyo wakiwa kwenye hali gumu.
60. _____ Ninaweza kupambanua ukweli au uongo.
61. _____ Mimi huwa tayari kuamini kuwa Mungu atatuongoza kwa hali ambayo wengine wanahisi haiwezekani.
62. _____ Watu hujihisi nyumbani wanaponitembelea.
63. _____ Mimi hupenda kutengeneza vitu kwa mikono yangu.

64. _____ Mungu hujibu maombi yangu kwa njia dhahiri.
65. _____ Nimewahi kumobea mgonjwa ya kuwa Mungu amrejeshee afya yake nae akapata nafuu.
66. _____ Nina uwezo wa kufangamana na watu wanaotoka katika maeneo na tabaka mbalimbali.
67. _____ Mimi huidhamini fursa ya kutangaza neno la Mungu kwa wengine.
68. _____ Katika dunia ya leo ni muhimu kwangu kunena maonyo na hukumu ya Mungu.
69. _____ Ni furaha yangu kushiriki Kristo na jirani yangu asiye hudhuria kanisa.
70. _____ Watu hupenda kunielezea yanayowakera maana wao huhisi ya kuwa ninawajali.
71. _____ Kuwafunza watu kuwa Wakristo bora ni furaha yangu kuu.
72. _____ Nafahamu kuwa uweza wangu wa muziki utawafaidi watu.
73. _____ Watu ambao wanahisi kusongwa, mara nyingi huja kwangu kuwafariji na kuwatia moyo.
74. _____ Huhisi kuwa nina ufahamu wa kina kulitatua jambo ngumu.
75. _____ Ninaufahamu mwafaka kuhusu mafundisho ya Bibilia.
76. _____ Mimi hutosheka ninapoifanya kazi kuliko kumtafuta mtu mwingine kuifanya.
77. _____ Huidhamini huduma inayowasaidia watu wengine kubeba mizigo yao.
78. _____ Ni jambo la kuisimua ninapowachochea wengine kuhusika na kazi kanisani.
79. _____ Natosheka kuandaa ratiba ya utendakazi kanisani.
80. _____ Ni furaha kuona kiasi cha fedha ninachoweza kumtolea Bwana.
81. _____ Hufurahia kumhudumia mgonjwa hospitalini.
82. _____ Ninaweza kupambanua yaliyo ya ukweli na yasioyo ya kweli kwenye usemi wa kitheolojia.
83. _____ Watu hunitazama kama mtu anayeamini chochote chawezekana.
84. _____ Wamishonari watakapo kuja kwetu kanisani ningependa wanitembelee kwangu nyumbani.
85. _____ Nimeona matokeo ya kufanya kazi na vitu alivyounda Mungu, na nimeboresha na kurembesha kile watu wengine hawajaona au kuendeleza.
86. _____ Mimi huwaombea wengine kwa uaminifu nikitambua ya kuwa maombi yangu husababisha mafanikio yao.
87. _____ Hupenda kuwahudumia wapungufu kifedha au kihisia na kuwaombea urejesho wa afya zao.
88. _____ Wazo la kuanzisha kanisa jipya kwa jumuiya mpya linanisisimua.
89. _____ Ninapenda kuwafunza watenda kazi kanisani.
90. _____ Ninapo funza katika darasa la Bibilia ni muhimu kushiriki neno la Mungu hata kama wengine hukwazwa.
91. _____ Nina mzigo mkubwa kwa watu ambao hawaja fikiwa na injili kwa jumuiya yangu.
92. _____ Hufurahia mahusiano ya karibu na watu haswa mmoja kwa mwingine.
93. _____ Ni rahisi kwangu kuandaa mafunzo ya kufundishia darasa la Bibilia.
94. _____ Kuwaongoza wengine kuimba nyimbo za sifa kwa Mungu ni jambo linalonipa kutosheka kibinafsi.
95. _____ Ni heri kuikaribisha jamii isio na makaazi rasmi kanisani kuliko kukaribisha jamii nyingine ambayo haihudhuria kanisa.
96. _____ Nina ujasiri mkubwa ninapotatua shida zangu.
97. _____ Ninasisimka kusoma na kuchambua kitabu kigumu katika Bibilia.
98. _____ Hupenda kufanya kazi bila ya kutaka sifa.
99. _____ Mimi hupenda kusaidia jamii ambazo zinapitia hali ngumu.

100. _____ Afadhali kufanya uamuzi wakuliko kukishawishi kufanya uamuzi.
 101. _____ Ninaweza kutoa kwa kujinyima maana ninajua Mungu atosheleza mahitaji yangu.
 102. _____ Naridhika pakubwa ninapowatembelea waliolazwa nyumbani.
 103. _____ Mara nyingi mtu anapoongea, ninachunguza nia yake.
 104. _____ Watu wanapokufa moyo mimi hufurahia kuwainua / kuwapa matumaini.
 105. _____ Watu hufurahia kutembea nyumbani kwetu.
 106. _____ Ni furaha yangu kuchora, kuunda au kupaka rangi vyombo tofauti.
 107. _____ Hujipata naomba badala ya kufanya shughuli nyingine.
 108. _____ Nahisi kwa nguvu ya kwamba maombi yangu kwa mgonjwa.
 109. _____ Zaidi ya yote nina shauku kubwa kuona watu wa jamii nyingine na mataifa wakimgeukia Bwana.
 110. _____ Zaidi ya yote, natamani kuona watu wa jamii nyingine na mataifa wakimpokea Bwana.

Hongera, umekamilisha zoezi la karama za kiroho.

Tafadhali chukua muda kutazama maswali yote ili kuhakikisha ujasahau kujibu lolote. Sasa hamisha majibu yako kwenye karatasi ya uchambuzi, ili kufanya hivyo, lazima uyatazame majibu yako kwa kila swali.

Kwa kila mmojawapo ya maswali 110 (mia moja na kumi) jaza jibu lako la nambari katika kijisanduku. Kisha ongeza idadi ukianzia juu na kuteremka na baadaye idadi kamili kwenye kijisanduku, huu ni mfano kwa kifupi.

Swali	Jibu	Swali	Jibu	Swali	Jibu	Swali	Jibu	Swali	Jibu	Swali	Jibu	Cheo	Karama za Kiroho
	1		3		0		1		3		8	2	Mtume
	3		1		1		0		1		6	3	Nabii
	3		5		3		5		1		17	1	Mwinjilisti

Sasa angalia **idadi zote**, idadi ya juu huenda ikawa ndio **kipawa cha Kiroho** kilicho na nguvu ndani yako. Watu wengine watakua na karama tofauti zinazolingana kwa idadi. Tathmini hii sio timilifu. Kwa hivyo labda karamu yako yenye nguvu zaidi isijionyeshe kwenye jumla ya juu mwisho utapata orodha ya karama zo kiroho ikikupa andiko linaloandamana na kila mojawapo.

Hivi vipawa vya kiroho vinaweza kupatikana katika tovuti
<http://www.kodachrome.org/spiritgift>

Karama za kiroho

Usitazame kwenye karatasi hii kabla ya kumaliza mthani

Swali	Jibu	Swali	Jibu	Swali	Jibu	Swali	Jibu	Swali	Jibu	Jumla	Nambari	Vipawa vya Kiroho
1		23		45		67		89				Mutume
2		24		46		68		90				Nabii
3		25		47		69		91				Mwinjilisti
4		26		48		70		92				Mchungaji
5		27		49		71		93				Mwalimu
6		28		50		72		94				Nyimbo
7		29		51		73		95				Kuinua
8		30		52		74		96				Hekima
9		31		53		75		97				Maarifa
10		32		54		76		98				Kuhudumu
11		33		55		77		99				Kusaidia
12		34		56		78		100				Uongozi
13		35		57		79		101				Kusimamia
14		36		58		80		102				Kutoa
15		37		59		81		103				Huruma
16		38		60		82		104				Mbambanua
17		39		61		83		105				Imani
18		40		62		84		106				Mapokezi
19		41		63		85		107				Ubunifu
20		42		64		86		108				Maombezi
21		43		65		87		109				Uponyaji
22		44		66		88		110				Umishonari

Orodha ya vipawa vya Kiroho

Mtume

Hii ni karama ambayo Roho Mtakatifu huwachagua Wakristo fulani, kuongoza, kusaidia na kukuza makanisa ya Mungu kwa kutangaza na kufundisha mafundisho ya kweli. Tazama **Matendo ya Mitume 12 :1-5, 14 :21-23.**

Nabii

Ni karama maalum ambapo Roho Mtakatifu huwawezesha baadhi ya Wakristo kutafsiri na kutumia ufunuo wa Mungu liwe katika utendaji juu ya swala fulani. Tazama **1 Wakorintho 14 :1-5 , 14 :30-33, 14 :37.**

Mwinjilisti

Ni karama inayopeanwa na Roho Mtakatifu kwa baadhi ya Wakristo kushiriki ao kueneza injili kwa wasioamini ili wafanyike wanafunzi wa Bwana Yesu Kristo. **Matendo ya Mitume 8 :26-40.**

Mchungaji

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani ili kuchukua jukumu la kiroho la uwajibikaji juu ya kikundi cha waumini. **Tazama 1 petero 5 :1-11.**

Mwalimu

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo kushiriki ukweli wa neno, ili watu wapate kujifunza. **Tazama Waebrania 5 :12-14.**

Muziki

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani kumsifu Mungu kupitia njia tofauti za miziki na kuboresha hali ya ibada katika kusanyiko. Tazama **1 Wakorintho 14 :26, Marko 12 :36.**

Kuinua

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani ili kuleta faraja na ushauri kwa watu walio kwenye hitajii ili wasaidike. Tazama **Matendo ya Mitume 11 :23-24, 14 :21-22.**

Hekima

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani kuelewa mapenzi ya Mungu na yanavyohusiana na maisha. **Yakobo 3 :13-17.**

Maarifa

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani kuelewa kwa njia ya kipekee mapenzi ya Mungu na jinsi yawezavyo kutumika katika hali tofauti kanisani. Tazama **Waefeso 3 :14-19.**

Kutumika

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani kubeba mizigo ya Wakristo wengine na kuwasaidia ili watende kazi zao kwa njia ya ubora zaidi. Tazama **Wagalatia 6 :1-2.**

Usaidizi

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwapa Wakristo fulani ili waweze kubeba mizigo ya Wakristo wenzao kikamilifu. Tazama **Matendo ya Mitume 6 :2-4.**

Uongozi

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani kuchochea, kuelekeza na kusaidia Wakristo ili wajitolee na kufanya kazi ya Mungu kanisani pamoja. Tazama **Waebrania 13 :10, Kutoka 18 :13-16.**

Usimamizi

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo fulani kuchochea, kuelekeza na kusaidia Wakristo ili wajitolee na kufanya kazi ya Mungu kanisani pamoja. Tazama **Waebrania 13 :10, Kutoka 18 :13-16.**

Usimamizi

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu hupeana. Karama hii huwawezesha baadhi ya Wakristo kuelewa malengo ya huduma kanisani na huelekeza kutenda jambo hilo kwa ukamilifu, kwa kuweka kanisa kwa mwelekeo. Tazama **Matendo ya Mitume 12 :12-21**.

Kukitimu

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo kutoa mali yao kwa kazi ya kanisa kwa njia kubwa wakiwa na furaha. Tazama **2 Wakorintho 8 :1-15**.

Rehema

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo baadhi ya Wakristo kuhisi huruma kwa wale wanaoteseka na kumia na wao hujitolea kwa hali na mali ili kuondoa huzuni ya wanaohitaji. Tazama **Luka 10 :30-37**.

Kupambanuwa

Hii ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo baadhi ya Wakristo kuelewa ikiwa tabia imetokana na Mungu au Shetani. Tazama **Matendo ya Mitume 16 :16-18**.

Imani

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha baadhi ya Wakristo kuwa na ujasiri kuhusiana na ahadi, nguvu na uwepo wa Mungu ili waweze kusimamia kishujaa makazi ya Mungu iendelee. Tazama **Waebrania 11**.

Mapokezi

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha baadhi ya Wakristo kufungua nyumba zao kwa kupeana chakula, malazi na ushirika kwa furaha. Tazama **Mwanzo 18 :1-15**.

Kipawa

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha baadhi ya Wakristo uwezo wa kutumia mikono yao kujenga ufalme wa Mungu kupitia uimbaji wa Kibinafsi. Tazama **Kutoka 28 :3-4**.

Maombezi

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha baadhi ya Wakristo kuomba na kuna matokeo makumbwa ya ujenzi wa ufalme. Tazama **1 Thesalonike 3 :10-13, 1 Timotheo 2 :1-2**.

Uponyaji

Ni karama maalum ambayo Roho Mtakatifu huwatumia Wakristo kurejesha afya kwa wagonjwa. Tazama **Yakobo 5 :13-16, Luka 9 :1-2**.

Umishonari

Ni karama maalum inayopeanwa Roho Mtakatifu kwa baadhi ya washirika wa mwili wa Kristo ili kuhudumu kwa vipawa walivyo navyo katika eneo tofauti au jumua. Tazama **1 Wakorintho 9 :19-23**.

Sura ya Sita

USIMAMIZI WA WATU

***“Nakama mnavyotaka watu wawatendee ninyi, watendeeni vivyo hivyo.”
Luka 6:31***

Amri kuu. Sote twaifahamu vyema amri hii lakini mara nyingi inatushinda kuitimiza. Kanisa linahusu watu na hujengwa juu ya mahusiano – na Mungu pamoja na watu wengine. Yesu alitufundisha kanuni hii ili tuweze kuishi kwa amani mmoja kwa mwingine, na pamoja na Mungu ili tudhihirishie ulimwengu ambao Yesu alifia ili utambuwe upendo wake. Unapowasimamia watu shirikiana nao wala usiwe tu mtawala juu yao. Usimamizi wa watu sio kuwaambia kile wanatakiwa kukufanyia bali kuwauliza wao kitu ambacho unaweza kuwatendea. Kama vile Yesu alivyotufundish hili litakuwa ni zoezi la kila siku la amri kuu. Katika sura hii tutatazama umuhimu wa usimamizi wa watu, baadhi ya kanuni za usimamizi na jinsi ya kuwasimamia watu.

I.KWA NINI USIMAMIZI WA WATU NI MUHIMU ?

1. Kanisa linahusu watu

“Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate zitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.” 1 Petro 2:9

- Kanisa sio jengo, ni watu
- Lengo letu linawahusu watu sio vitu
- Yote yanahusu uhusiano
 - Na Mungu
 - Pamoja Kristo
 - Mmoja na mwingine

2. Watu ndio raslimali kuu ya kanisa

- Watu ndio raslimali kubwa ya kanisa
- Watu huleta ujuzi na vipawa vingi kanisani

“Lakini kila mmoja hupewa ufunuo na Roho kwa kufaidiana.” 1 Wakorintho 12:7

 - Vipawa vya kiroho kwa huduma
 - Ujuzi kwa ajili ya huduma
- Kuwekeza kwa watu huleta matokeo makubwa baadaye.

3. Huduma hutendeka kupitia watu

“kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye Yule azitendaye kazi zote katika wote.”1 Wakorintho 12:6

- Watu hufanya huduma na kuhudumiwa pia
- Raslimali nyingine (ni vifaa) vya kuwasaidia watu
- Huduma ya Yesu ilihudumia mioyo ya watu

4. Washirika wa kanisa wamejitolea, si waajiriwa

- Wenye kujitolea wanahitaji kupewa motisha
 - Lazima wahisi wanaongozwa na Mungu
 - Pasipo na msukumo, hapana kusudi na basi watu hawapo
- Wenye kujitolea wanahitaji kutiwa moyo.
 - Waliojitolea wanahitaji hakikisho kuhusiana na wanayotekelezwa
 - Waliojitolea wanahitaji kufanya kazi kikamilifu
- Waliojitolea wanahitaji kupewa motisha
 - Hawalipwi kwa hivyo wanahitaji jambo la kuwafanya waendeleo
 - Motisha wao utokane na injili

5. Kuepuka Migogoro

- Migogoro katika kanisa hutokea kati ya watu
- Kujifunza jinsi ya kukabiliana na watu kwenye mgogoro ni ya muhimu

II. KANUNI ZA USIMAMIZI WA WATU

1. Watu ni wa kipekee

“Maana wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu, uliniunga tumboni mwa mama yangu.”Zaburi 139:13

- Wana ujuzi wa kipekee
- Wana uzoefu wa kipekee
- Wana maoni ya kipekee
- Wana haiba ya kipekee

2. Watu wanataka kuwa sehemu ya jambo

- Watu hupenda kuhisi ya kuwa hao ni sehemu ya jambo fulani
- Watu hawapendi upweke

“Bwana Mungu akasema, si vyema huyo awe pekee yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.”Mwanzo 2:18

- Yesu alitambua haja yetu ya ushirika.

3. Watu wanataka kuhusika

- Watu wana hamu ya kuhusika wala sio kutazama tu
- Watu wana hamu ya kuchangia
- Watu wangependa kutumia vipawa na ujuzi walio nao panavyohitajika

4. Watu wanataka kudhaminiwa

- Lazima watu wajihisi wana umuhimu
“Nakusihi kwa ajili ya mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu, yaani, Onesmo, ambaye zamani alikuwa hakufai, bali sasa akufaa sana, wewe na mimi pia.”Filemoni 1:10-11
- Ikiwa watu watadhaminiwa watajitolea

5. Watu wanataka heshima

“Waheshimu watu wote.” - 1 Petro 2:17

- Watu wanataka wapokelewe kwa heshima
- Mungu anawajali watu, lazima nasi tuwajali

6. Watu wanataka kutambuliwa

“Ninafurahi kwa sababu ya kuja kwao Stephana na Fortunatu na Akaiko; maana kuwa wamenikirimia kwa wingi yale mliyopungukiwa kwenu. Maana wameniburundisha roho yangu na roho zenu pia basi wajueni sana watu kama hao.”1 Wakorintho 16:17-18

- Watu wanahitaji shukurani
- Utambuzi huleta ujasiri

7. Watu wanataka mwelekeo

- Shiriki maono
 - Kama kiongozi, lazima uwape wengine motisha
 - Hakikisha kila mmoja analenga kwenye lengo kuu
“Pasipo maono watu huacha kujizuia.”Mithali 29:18
- Ratibu jitihada
 - Hakikisha kuwa watu wanafanya kazi pamoja
 - Usiruhusu shughuli uzisosifahamu au zisizohusiana na maono au malengo ya kanisa
- Tumia mtindo wa uongozi ulio bora zaidi
 - Tumia mtindo tofautiinayohitajika kwa maeneo tofauti
 - Wape majukumu na wajibu unao hitajika

8. Watu wanataka habari

- Wasilisha malengo yako na matarajio
- Hakikisha kila mtu anaelewa majukumu yake
- Usidhani watu wanaelewa jambo fulani waeleze
- Shiriki habari muhimu kuhusu swala

III. KUSIMAMIA AINA TOFAUTI YA WAFANYAKAZI KANISANI

1. Kusimamia walioajiriwa kanisani

- Ni sehemu ya kikundi chako cha huduma, kuwa mkarimu na uwaunge mkono
- Utahitajika kuwapa majukumu kutekeleza wala sio shughuli tu
- Kufanya kazi kwa pamoja
- Kila mmoja atahitaji maeneo ya wazi ya wajibu na mamlaka

2. Kusimamia viongozi kanisani

- Wape majukumu maalum ya kulenga au kuhudumu
- Kudumisha mamlaka yako na udhibiti wote kama kiongozi
- Peana mwelekeo na usaidizi
- Endelea kutoa mafunzo ya mara kwa mara
- Uwe na umakini dhidi ya wanaotaka vurugu katika huduma yako
 - Watu wanaotaka kufanya mambo kivyao
 - Watu wasiotaka kunyenyekea chini ya mamlaka yako

3. Kuwasimamia wanaojitolea

- Uwe mwenye kuwatia moyo na kuwafariji
- Weka malengo maalum kwa ajili yao
- Wape majukumu yakiwa na tarehe ya kufuatilia kukamilka, ili kuhakikisha yametekelezwa
- Toa ushauri kwa viongozi wa baadaye
- Himiza uvumbuzi au mawazo mapya
- Wape kiongozi atakayewasimamia moja kwa moja

Zoezi la Kusimamia Watu

Maelezo: Kwa kila hali iliyo kwenye mikono wa kushoto, andika kanuni mwafaka ya usimamizi wa watu itakayotumika.

Hali	Kanuni ya usimamizi wa watu
1. Mshirika wa kanisa amekuja kwako akisema anataka kuhudumu kwa kikundi cha kuongoza ibaada	
2. Mmoja wa viongozi wako amekuomba majina ya washirika wote na vipawa vya kiroho walivyo navyo.	
3. Familia moja imehama kanisani na wamekueleza ya kwamba hawakujua yeyote kanisani.	
4. Vijana kanisani mwako hawana furaha, kwa sababu hakuna anayejali maombi yao ya raslimali.	
5. Kiongozi wako wa huduma ya watoto anataka kujua jinsi huduma yao inachangia kwa maono ya kanisa.	
6. Watu wanasita kujitolea kwenye mradi kanisani.	
7. Viongozi wawili wa huduma kanisani hawaelewani kuhusu jinsi ya kutimiza lengo la kanisa	
8. Kiongozi aliyejitolea kwa muda mrefu katika huduma ya watoto amekoma ghafla kuhudumu.	

Sura ya Saba

KUTATUA MIGOGORO

“Heri wapatinishi maana hao wataitwa wana wa Mungu.” Mathayo 5:9

Kiongozi yeyote lazima aelewe ya kuwa mgogoro ni lazima katika shirika lolote lile linalohusisha watu. Kama tulivyosema awali, kanisa linahusu watu na uhusiano kati ya watu hao. Ugomvi na Mungu ni dhambi. Kutoelewana na wenzetu pia kunaweza kutuingiza kwenye dhambi, lazima tuwe na tahadhari tusije tukanasa katika dhambi. « ile utuzingayo kwa upesi » kama inavyosema Bibilia katika Waraka wa *Waebrania 12:1*. Yesu kwenye ujumbe wake alipohubiri akiwa mlimani, katika *Mathayo 5:9* alisema « Heri wapatinishi maana hao wataitwa wana wa Mungu » Yesu ametuita sote kuwa wapatanishi, na kwa sababu mgogoro utatokea, lazima tujiandae kukabiliana nao kulingana na Bibilia. Katika sura hii tutazungumzia umuhimu wa kukabiliana na migogoro, viini na sababu zinazochangia na jinsi ya kutatua migogoro, kimaandiko.

I. Je, kuna umuhimu upi katika kutatua migogoro?

1. Migogoro huwa kanisani kila wakati
 - Unapohusiana na watu, hapakosi migongano.
 - Ukweli haubadiliki lakini watu huelewa jambo kwa njia tofauti.
2. Matatizo mengi kanisani huchangiwa na kutoelewana
 - Migogoro inaweza kuliingilia kanisa na kulizuia kukua.
 - Mambo madogo yanaweza kuzusha mgogoro mikubwa
3. Migogoro inaweza kulivunja au kuligawanya kanisa

“Na nyumba ikifitinika juu ya nafsi yake, nyumba hiyo haiwezi kusimama.”
Mariko 3:25

 - Kwa kuwa na vikundi au mitazamo tofauti
 - Kwa kudunisha mamlaka yako
4. Kutatua migogoro kwa njia mwafaka hulisaidia kanisa kusonga mbele.
 - Ondoa vizuizi vya kuendelea mbele
 - Jenga mfumo wa ufahamu na mbinu za kutatua mgogoro.

II. Viini vya Migogoro

1. Kati ya washirika

- Mitazamo tofauti ya mambo
- Uzoefu tofauti
- Malengo na jinsia tofauti

2. Kati ya mchungaji na washirika wa kanisa

- Malengo tofauti
- Nia tofauti
- Mitindo tofauti

3. Mtazamo kati ya mambo ya kale na ya kisasa

- Utaratibu dhidi ya uhuru
- Faraja dhidi ya umuhimu
- Msimamo dhidi ya ulegevu

4. Kati ya vizazi

- Sasa dhidi ya zama zile
- Ujana dhidi ya uzee
- Wanaozungumza dhidi ya wanyamavu

5. Kati ya huduma

- Kushindania raslimali
- Kushindania watu
- Kushindania kutambulika

III. Kinachosababisha Migogoro

Mgogoro wowote una kiini ao sababu na hutoka kwenye sehemu tatu:

1. Shetani

- Yeye yupo na kila mara anataribu ili tutende dhambi

*“Muwe na kiasi na kukesha kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba agurumaye, huzunguka zunguka, akimtafuta mtu ammeze”*1 Petro 5:8

2. Asili yetu ya dhambi

- Tumezaliwa wenye dhambi. Hii ndio asili yetu.

*“Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na roho, na roho kushindana na mwili, kwa maana hizi zimepingana hata hamwezi kufanya mnayo taka.”*Wagalatia 5:17

3. Ulimwengu wenye dhambi

- Ulimwengu umeja ufisadi na utajaribu kutuingiza kwenye ufisadi

*“Maana kila kilichomo duniani, yaani tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba bali vyatokana na dunia.”*1 Yohana 2:16

IV. Sababu zinazoleta migogoro

1. Maono na malengo ambayo hayajawekwa wazi na kutokuwa na kipindi cha maombi, kutafakari na majadiliano.
 - Vikundi au watu wenye maono au malengo yanayogongana
 - Pasipo maono kabisa

“Pasipo maono watu huwacha kujizuia.”Methali 29:18
2. Kukosa mpango wa kimkakati
 - Hakuna mpango maalum uliyowekwa ili kuhakikisha ya kuwa rasilimali zimengawanywa kulingana na umuhimu.
 - Watu wanang’ang’ania rasilimali bila kujali mahitaji ya kikundi.
 - Watu wanang’ang’ania rasilimali wakiegemea mahitaji ya muda bila kujali siku zijazo.
 - Hamna mpango madhubuti kuhusu rasilimali za kanisa.
3. Ufunzi usio mutimilifu
 - Watu hawajafunzwa kanuni za Kristo
 - Maadili ya kiKristo hayajaonyeshwa na uongozi wa kanisa
 - Ukosefu wa kutatua migogoro kimaandiko
4. Mawasiliano mabaya
 - Watu hawajui mahitaji mengine ya kanisa
 - Mawasiliano kutendeka baada ya wala si kabla ya
5. Kutokabiliana na matatizo
 - Migogoro ya awali haijatatuliwa
 - Matatizo yaliyoko kupuuzwa
 - Matatizo yanayoweza kuchipuka hayatarajiwi

V. Kutambua Migogoro

1. Ishara za wazi
 - Maongeo ya hasira
 - Malalamishi yaliyonakiliwa
 - Umbeya na masengenyo
2. Ishara zisizokuwa za wazi (za kutahadharisha)
 - Kujitenga kutokana na shughuli za kanisa
 - Kuchelewa kwa miradi
 - Kutokuwa na mawasiliano

VI. Kutatua Migogoro

“Na ndugu yako akikukosea enenda ukamwonye wewe na yeye peke yenu, akikusikia, umempata nduguyo. La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena watu mmoja au wawili, ili kwa vinyua vya mashahidi wawili au watutu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza wao liambie kanisa; na asipo lisikiza kanisa pia na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru.”Mathayo 18:15-17

1) Ukiwa na mgogoro na mtu mwingine:

“Au utawezaje kumwambia ndugu yako, ndugu yangu, niache nikitoe kibanzi kilicho ndani ya jicho lako, nawe huiangalii ile boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe, ndipo utakapoona vyema kukitua kile kibanzi kilicho katika jicho la ndugu yako.”Luka 6:42

1. Tambua makosa yako kwenye mgogoro
 - Kibinafsi ujichunguze na utambue jinsi ulivyochangia katika mgogoro (kwa mfano maneno makali, lugha chafu, kukosa subira na kadhalika)
2. Kwanza kubali na uungame sehemu ya mgogoro unayohusika nayo
 - Unapomkabili mtu mliyefarakana naye, nenda ukiwa na nia hii.
3. Omba msamaha kwa makosa yako
Ukisha kuomba msamaha kwa makosa uliyotenda na ukapokea msamaha, sasa unaweza kuwaeleza kuhusu waliyokutendea.
4. Kama msamaha umetolewa, mgogoro wako umetatuliwa
5. Ikiwa yule mtu mwingine hatakusamehe, pata mtu mmoja au zaidi kulingana na **Mathayo 18:15-17**

2) Unapoitwa kupatanisha mgogoro

1. Tambua mgogoro
 - Litambue tatizo lenyewe
 - Hakikisha kila mhusika anafahamu na kuelewa shida ni ipi na kila mmoja anahusika vipi. Ikiwezekana, andika chini dhambi zilizotendwa ili wasemeheane moja baada ya nyingine.
2. Watambue wahusika
 - Tambua haswa ni nani anahusika
 - Tambua jinsi wanavyohusika (dhambi zao ni zipi?)
 - Tambua kwa nini wanahusika

3. Tatua ki – maandiko
 - Mtukuze Mungu kwa yote utendayo
 - Ruhusu kila mhusika akubali na aungame makosa yake (**Luka 6:42**)
 - Acha kila mmoja wao aombe msamaha.
 - Ikiwa msamaha haujatolewa, basi chukua hatua ya mashahidi (**Mathayo 18:15-17**).

4. Tatua kwa amani
 - Migogoro huleta fursa
 - Usitende dhambi unapojaribu kutatua migogoro
 - Usiharibu mambo kwa kudhania, pata habari kamili
 - Zikumbuke amri zilizo kuu.
 - Mpende Mungu
“Akawaambia, mpende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote” Mathayo 22-37

 - Mpende jirani yako
“Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako.”
– **Mathayo 22:39**

VII. Baada ya mgogoro

1. Tunawajibika tu kwa matendo yetu wenyewe
 - Ishi kwa hekima
“Basi angalia sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima.” Waefeso 5:15

 - Mungu pekee ndiye anayeweza kugeuza mioyo
“Na Roho wa Bwana atakujia kwa nguvu nawe utatabiri pamoja nao, nawe utageuka kuwa mtu mwingine” 1 Samweli 10:6

2. Msamaha ni nguvu
 - Weka migogoro nyuma yako
 - Kwa maneno ya Yesu “enenda na sitende dhambi tena“
“Wala mimi sikuhukumu, enenda zako; wala usitende dhambi tena”
– **Yohana 8:11**

3. Uwe mpatanishi

“Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu.” - Mathayo 5:9

VIII. Mgogoro huwa sio mbaya kila wakati

1. Inawezekana kuwa na mgogoro bila dhambi (maoni yanaweza kuwa tofauti. Jinsi ya kutatua shida fulani. Wote wakishirikiana kupata matokeo bora ya kufaidiana)
2. Mgogoro unaweza kutambua pengo linalohitaji kuzibwa, (kwa mfano kulipa jambo umakini zaidi au maelezo zaidi).

Zoezi la Kukabiliana na Mgogoro

Mifano ya migogoro kanisani	Suluhisho
1. Viongozi wa huduma ya vijana hawajaridhika na raslimali na nafasi waliotengewa, wanasema wanahitaji zaidi.	
2. Bodi ya wazee haikubaliani na mchungaji kuhusu mwelekeo mpya wa kanisa	
3. Baadhi ya washirika wa zamani kanisani wameanza kulalamika kuhusu nyimbo geni za kuabudu, wamataka kutumia nyimbo za zamani.	
4. Familia mbili katika kanisa lako zinafarakana kuhusu ardhi kisheria na washirika wameanza kuwaunga mkono.	
5. Kuna uvumi kuwa kiongozi wako wa ibada anashiriki kwenye tendo la usherati.	

Sura ya Nane

KUFANYA WANAFUNZI

“Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.” – Mathayo 28:19

Kanisa lilianzishwa duniani kuwavuta watu ili wahusiane na Mungu kupitia Yesu Kristo. *“Maana Mungu hakumtuma Mwana wake ulimwenguni ili ahukumu ulimwengu, bali ulimwengu utolewe na yeye.”*(Yohana 3:17). Kuwa viongozi wa kanisa kazi kuu sio kulisimamia kanisa bali ni kuwanongoza wengine kwa Kristo. Tunaliita jambo hili kufanya wanafunzi. Tuwe tunahubiri, kufunza, kuvua nafsi au kuabudu, ni ya muhimu ya kuwa nia yetu iwe ni kuona “Kristo akiumbika ndani ya wengine.” (Tazama **Wagalatia 4:19**). Katika sura hii tutazungumza kuhusu Kiwanafunzi, kusudi lake, kanuni na utenda kazi na umuhimu wa kuwatathmini.

Je tofauti kati ya kufundisha na kufanya uanafunzi ni ipi?

- Kufundisha ni kupokeza maarifa au habari. Inahusisha ufahamu
- Uanafunzi ni utekelezwaji wa maarifa/ mafunzo. Inahusisha utendaji

I. KUSUDI LA UANAFUNZI

1. Kuona Kristo akiumbika ndani ya wengine

*“Vitoto vyangu ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu.”*Wagalatia 4:19

- Hili ndilo lengo la kanisa
- Mbingu yote hufurahi wakati mototo mmoja aliyepotea hupatikana
*“Nawaambia, vivyo hivyo kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye.”*Luka 15:10

2. Ili kukuza karama za kiroho za wengine

*“Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.”*1Wakorintho 12:7

- Kuchochea karama walizo nazo washirika wako
- Kuzitumia karama zilizopo ndani ya washirika

3. Ili kufunza na kuwapa ujuzi wengine kwa kazi ya huduma

“Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.”

2 Timotheo 3:16-17

- Huduma kwa washirika wa kanisa
- Huduma kwa walio nje ya kanisa

4. Kukuza kanisa
 - Wanafunzi huwafanya wanafunzi wengine
“Basi enendeni mkawafanye wanafunzi wa mataifa yote...” Mathayo 28:19
 - Kuendeleza huduma yako kwa watu zaidi
5. Ni ya muhimu kuwakuzu viongozi wengine
 - Walio na uwezo wa kufanyika viongozi lazima kwanza wapewe nidhamu
 - Imani dhabiti ni kigezo muhimu kwa viongozi

II. KANUNI ZA UANAFUNZI

1. Kazi ya kuwafanya watu kuwa wanafunzi kamwe haishi
“Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo tukaze mwendo ili tuukilie utimilifu.” Waebrania 6:1
 - Hakuna kufuzu kamwe katika uanafunzi
 - Safari ni ya muhimu kama vile mwisho wa safari hiyo
2. Ni kipaumbele cha kanisa
“Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Roho Mtakatifu” Mathayo 28:19
 - Kanisa lilitengenezwa kwa makusudi haya
 - Kilia kitu kanisani hufaidika kwa makusudi haya
 - Watu wanapofunzwa kuwa wanafunzi watatumika zaidi
 - Watu wanapofunzwa kuwa wanafunzi watashiriki zaidi
 - Watu wanapofunzwa kuwa wanafunzi watatoa zaidi kanisani
3. Kufanyika mwanafunzi huchukuwa muda
 - Haifanyiki mara moja tu
 - Utaupandaje mlima? – Hatua baada ya hatua
4. Kufanyika mwanafunzi hugarimu jitihada
 - Watu wanahitaji kusaidiwa
 - Watu wanahitaji kutiwa moyo
 - Watu wanahitaji uwajibikaji
5. Kufanyika mwanafunzi kunahitaji watu
 - Sajili watu wengine kusaidia katika kufanya washirika wako kuwa wanafunzi
 - Shuhuda ni vifaa bora zaidi
 - Kila Mkristo anahitaji ndugu au dada wakutembea naye

“Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwingie wa kumwiinua” Mhubiri 4:10

6. Kufanyika mwanafunzi kunagarimu shauku
 - Lazima utamani *“kuona Kristo akiumbika ndani ya wengine”*Wagalatia 4:19
 - Kila mmoja wetu ni lazima atamani kukuwa kwa imani yake
*“Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi”*Waraka wa Yokobo 4:8

III. MCHAKATO WA UANAFUNZI

A. Ishara za Uanafunzi ni zipi?

1. Imani

“Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona” 2 Wakorintho 5:7

- Mwanafunzi hutembea kwa imani
- Mwanafunzi humtumainia Mungu
- Mwanafunzi hushikilia imani yake hata nyakati za shida

2. Ibada

“Akawamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa akili zako zote” Mathayo 22:37

- Mwanafunzi hutambua kuwa Mungu ni Mkuu
- Mwanafunzi humpa Mungu utukufu kila mara
- Mwanafunzi uhudhuriaibada kila wakati

3. Kusoma Bibilia

*“Kila andiko, lenye punzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadhibisha katika haki ili mtu wa Mungu awe kamili, apate kutenda kila tendo jema”*2 Timotheo 3:16-17

- Mwanafunzi hujifunza njia za Mungu kila mara
- Mwanafunzi hutamani hekima yake Mungu
- Mwanafunzi hatafuta majibu katika neno laMungu

4. Maombi

“Ombeni bila kukoma” 1 Wathesalonike 5:17

- Mwanafunzi huongea na Mungu kila siku
- Mwanafunzi huishi katika Roho Mtakatifu
- Mwanafunzi hugundua mpango wa Mungu katika maisha yake

5. Huduma

“Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana”

1 Wakorintho 15:58

- Mwanafunzi hutumikia mwili wa Kristo
- Mwanafunzi huwahudumia wengine kwanza
- Mwanafunzi huiga mfano wa Yesu

6. Misheni (Ujumbe) na Kushuhudia

“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa Nchi” Matendo ya Mitume 1:8

- Mwanafunzi hushuhudia yale Bwana ametenda
- Mwanafunzi huenda mahali Bwana anamwongoza
- Mwanafunzi hufanya watu wengine wanafunzi

B. Kutengeneza Mpango wa Uanafunzi

1. Tengeneza malengo ya uanafunzi
2. Tambua viongozi na waalimu
3. Kusudia na uwe na lengo la kulitekeleza
4. Tengeneza mbinu ya uanafunzi, kama iliyoko hapa chini

Hatua 1: Mwaliko wa kuabudu

- Yote yaanza kwa mwaliko wa kuabudu
- Waache wahisi uwepo wa Roho Mtakatifu
- Omba kwamba Roho Mtakatifu awaguse kwa njia ya kipekee
- Wanapoguswa watiye moyo kumpokea Kristo
- Watiye moyo kuungama imani yao hadharani

Hatua 2: wasajili katika darasa la Mafunzo ya Biblia

- Waingize katika darasa la mafunzo ya Biblia
 - Funza masomo ya kimsingi ya Kikristo
 - Funza jinsi ya kuishi kwa Imani
 - Funza mtazamo wa dunia wa Kibiblia
 - Watie moyo kusoma Biblia wenyewe

Hatua 3: Wahimize kuishi maisha ya maombi

- Andaa mafunzo ya maombi
- Wahusishe katika huduma za maombi

Hatua 4 : Wahusishe katika huduma

- Wanahitaji kutumika kanisani mwao
 - Wanahitaji kusimama na kanisa lao
 - Kama mshirika wa mwili wa Kristo ni ya lazima
- Waache wahudumu kulingana na uwezo wao
 - Kulingana na karama zao za kiroho
 - Karama zingine ambazo wako nazo

Hatua 5: Waongoze washirika katika huduma

- Wape nafasi za misheni
 - Kijijini
 - Kitaifa
 - Kimataifa
- Wape mafunzo ya uinjilisti
 - Andaa ushuhuda
 - Andaa majina ya watu ambao watashuhudiwa
 - Wafunze kuwa viongozi wa kanisa ama huduma

Hatua 6: Ongoza washirika kutoka kuwa wanafunzi na wafanye wanafunzi

- Watie moyo kuwakuza wengine
- Wafunze kuwafunza wengine

C. Tathmini Mnavyoendelea

- Kagua darasa lako
 1. Ni watu wangapi wanahusika kikamilifu katika mpangilio wa uanafunzi?
 2. Ni upande upi tunafanikiwa?
 3. Je washirika wetu wanakua katika imani yao?
 4. Je linazaa matunda kwa kanisa? Ama kwa mtu binafsi
 5. Ni athari zipi kwa kanisa/ jamii yetu?
- Fanya mabadiliko inayotakikana
 1. Tia moyo watu wahusike katika darasa ama kozi
 2. Tumia shuhuda kutia wengine moyo

Zoezi la Kufanya Wanafunzi

Maelezo: Jaza mapengo yaliyopo chini ukitumia mawazo na maoni yako mwenyewe, ukitathimini ni somo lipi lingefunzwa kanisani, wakati gani katika darasa la uanafunzi

• **Muumini mpya: Hatua 1 (Mwanzo wa imani)**

1. Mungu ni nani?	5.	9.
2. Ubatizo	6.	10.
3. Ushirika	7.	11
4. Mtazamo wa Biblia (AK na AJ)	8.	12.

• **Muumini aliyeokoka juzi: Hatua 2 (Msingi wa Imani)**

1. Mwanzo wa Umbaji	5.	9.
2. Karama za kiroho	6.	10.
3. Maisha ya kikristo AJ	7.	11
4. Utatu	8.	12.

• **Muunianayeimarika: Hatua 3 (Imani kukua)**


1. Historia ya Agano la kale	5.	9.
2. Shetani na maovu	6.	10.
3. Imani – Waebrania	7.	11
4. Ukuaji wa kiroho	8.	12.

• **Muumini Thabiti: Hatua 4 (Imani ya matendo)**

1. Kufunza neon	5.	9.
2. Huduma ya Uongozi	6.	10.
3. Misheni	7.	11
4. Ufunuo wa siku za mwisho	8.	12.

Sehemu ya Tatu

USIMAMIZI WA RASLIMALI



Sura ya Tisa

MPANGO WAKIMKAKATI

*“Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumaliza. Asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote waona wakaanza kumdhihaki
Luka 14:28-29*

Kuwa na mpango ni jambo lenye umuhimu mkubwa kwenye uongozi wa kanisa. Robert Schuller, mwandishi na mchungaji wa Crystal Cathedral, California anasema, “wanaokosa kupanga, wanapanga kushindwa”. Kuwa na mpango mwema hulisaidia kanisa hata kwa upande wa rasilimali ili zitumike vyema na katika kuyatimiza maono. Bila mpango makanisa hupoteza rasilimali na muda wa thamani na mwishowe hukosa kutimiza kile Mungu amewaitia kutenda. Bila shaka, kuwa na mpango hakulizuii kanisa kwa kutekeleza wajibu wake wa utendaji bali huweka msingi ambao kanisa linaweza kuutumia ili rasilimali zitumike kwa matokeo bora, katika sura hii tutajadili baadhi ya mambo yanayohusu mpango wa kimkakati na jinsi ya kuwa nao kanisa mwako.

I. Je, mkakati wa mpango ni nini?

- Mpango wa mbinu ni uwezo wa kupanga shughuli zako na malengo ili kutimiza maono.
- Mpango wa mbinu utakueleza rasilimali utakazoitumia, wakati wa kuzitumia na jinsi utakavyozitumia.

II. Kwa nini kanisa linahitaji mkakati wa mpango?

- Kutoa mwelekeo wa siku za usoni

“Na kwa nini mnaniita Bwana, Bwana, walakini hamyatendi msemayo? Kila mtu ajaye kwangu na kuyasikia maneno yangu na kuyatenda nitamwonyesha mfano wake, mfano wake ni mtu ajengaye nyumba, na kuchimba chini sana, na kuweka msingi juu ya mwamba ; na kulipokuja gharika, mto uliishukia nyumba ile kwa nguvu, usiweze kuitikisa kwa kuwa imejengwa vizuri, lakini Yule aliyesikia ila hakutenda. Mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba juu ya arthi pasipokuwa na msingi, mto ukaishukia kwa nguvu ikaanguka mara na maangamizi yake nyumba ile yalikuwa makubwa” Luka 6 :46-49

- Kuelekeza na kuongoza shughuli nyingi za huduma kanisani

- Kuepuka kuzubaiswa ovyo

- Kusaidia kulenga maono na malengo

Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazugukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii na tuweke kando kila mzigo mzito wa dhambi ile ituzingayo kwa upesi ; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyewekwa mbele yetu”

Waebrania 12:1

- Bila shaka kuepuka mambo ambayo yanatupotosha
- Kutumia rasilimali vyema na kwa njia bora
 - Kuwezesha ufanisi wa rasilimali zinazopotezwa
 - Kuongeza pato kutoka kwa rasilimali zilizopo
- Kuzuia migogoro ya baadaye
 - Kujiupusha na mgogoro kutokana na rasilimali zilizopo
 - Kujiupusha na malengo yanayotofautiana

III. Mkakati wa mpango unahusisha nini?

Kuna vipengele saba:

1. Taarifa ya maono

- Huelezea matokeo yanayotarajiwa
- Lengo lako kuu ni lipi?

2. Taarifa ya mahitaji

- Fafanua unayohitaji kutimiza kwenye maono
- Lenga kwa unachohitaji kutekeleza

3. Panga shughuli

- Tambua ni shughuli zipi utatumia ili kutekeleza kila haja
 - Elezea jinsi kila hitaji litatekelezwa
 - Wewe utafanya nini haswa
- Amua ni shughuli zipi au miradi ipi inatakikana ikamilishwe
 - Shughuli nyingine lazima zitapewa kipao mbele kuliko zingine
 - Shughuli nyingine zina umuhimu mkubwa katika huduma yako

4. Muda

- Huelezea wakati wa kutekeleza jambo
- Tambua wakati wa shughuli
- Tambua wakati shughuli inatakiwa kukamilishwa

5. Rasilimali

- Kipengele cha rasilimali kinazingatia kuulizia swala, **je** rasilimali tulizo nazo zitahitajika kutumika?
 - Huelezea wanachohitaji watu ili kutekeleza wajibu
 - Hutambua rasilimali zinazohitajika
 - Hutambua vifaa vinavyohitajika

- **Je ni raslimali zipi mpya zinazohitajika ?**
 - Majengo
 - Vifaa
 - Watu
- **Ni mafunzo yapi yanahitajika?**
 - Watu waongoze huduma
 - Watu wafanye huduma

6. Mbinu

- Tambua fursa za kipekee ulizo nazo
- Amua jinsi utakavyovitumia vipawa vya washirika wako
- Amua jinsi ya kuzitumia rasilimali ulizonazo kwa kuleta faida

7. Mipangilio

- Kuhusiana na maamuzi ya mradi
- Kwa maamuzi yanayohusu maswala ya fedha
- Amua ni nani atakayewajibika
 - Kuhakikisha malengo ya miradi yametimizwa
 - Kuhakikisha majukumu yametimizwa
- Tambua ni vikundi vipi vitahitajika na vitawahusisha kina nani

IV. Je, tutaunda mpango wa kimkakati kwa njia gani?

Hapa kuna hatua kadha za kimsingi zitakazo kuelekeza kuunda mpango wa kimkakati:-

1. kuandaa mpango wa kimkakati wa kikundi

- Wachague watu husika
- Wachague wenye ujuzi ufaao
- Waongeze wenye shauku kwenye mradi

2. Muhtasari wa mpango wako

- Kuanza na muhtasari rahisi
- Yaeleze maono yako na mahitaji muhimu

3. Ongeza habari zote muhimu kwa mpango wako

- Amua orodha ya shughuli utakazo tekeleza
- Eleza kwa undani vipengele vya kila shughuli
 - Muda
 - Rasilimali
 - Mbinu
 - Mpangilio

- Zingatia maoni yote ya kikundi au uwasilishaji wa maoni mapya
- Wacha mpango ubunike

4. Kusanya maoni kutoka kwa watu kanisani

- Kuongezea mpango au kuwasilisha maoni mapya
- Kupokea mitazamo tofauti ambayo inaweza kukusaidia
- Kukusaidia na kukuepusha usikwame ao kuwa na vizuizi katika mchakato wa mpango

5. Andika kwenye daftari

- Kuandika mpango kwenye daftari husaidia kuelezea
- Unaweza kusambaza kwa watu wengine ili watoe maoni yao
- Hutoa mwelekeo wa majadiliano
- Ni kitu dhahiri kinachoonyesha kuwa mpango umekuwepo

6. Kukamilisha mpango

- Tayarisha kwa kuandika mpango wako wa kimkakati
- Walio kwenye kikundi wauchunguze mpango huo kuanzia mwanzo hadi mwisho
- Mruhusu kila mtu kwenye kikundi aweke sahihi kwenye nakala
 - Kubali makubaliano
 - Kuepuka migogoro baadaye

7. Kuwasilisha mpango

- Wasilisha mpango wako kwa viongozi wakuu
- Wasilisha mpango wako kwa huduma ama washirika

ZOEZI LA MPANGO WA KIMKAKATI

Usemi wa Maono _____

Lengo 1 : _____

Shughuli :

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

Lengo 2 : _____

Shughuli :

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

Lengo 3 : _____

Shughuli :

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

Lengo 4 : _____

Shughuli :

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

Sura Ya Kumi

KUSIMAMIYA FEDHA

“Hamwezi kumtumikia Mungu na mali Mathayo 6:24

Karibu huduma zote zitahitaji fedha ili kutekelezwa. Kawaida watu hutegemea matoleo yanayotolewa na washirika. Kama kiongozi wa kanisa una jukumu la kuhakikisha ya kuwa pesa zote unazopokea zimenakiliwa inavyopaswa. Hili ni jambo unalotakiwa kulifanya kisheria lakini la muhimu zaidi, hii ni amri ya Biblia pia! Kusimamia vyema fedha za kanisa au huduma vizuri kunadhihirisha kwa Mungu na kwa washirika ya kuwa wewe ni mwaminifu. Biblia inatuonya ya kuwa tukikosa kuwa nakiwango cha juu cha uadilifu kifedha itatuletea uharibifu na mateso. Katika sura hii tutatazama usimamizi bora wa fedha unafaida gani? kanuni zake na jinsi ya kuwa na uadilifu wa kifedha pamoja na faida zake.

I. Kwa nini usimamizi bora wa fedha ni muhimu?

1. Biblia inasema ya kwamba pesa sinaweza kusababisha matatizo mengi
“maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha” 1 Timotheo 6:10

Usimamizi mubaya wa fedha huleta matatizo mengi

- Dhambi zingine (udanganyifu, kuiba, kutamani n.k)
“Haki humlinda yeye aliye mnyofu katika njia yake bali ubaya humwangusha mwenye dhambi.” Mithali 13:6
- Huharibu uhusiano
“Aendaye kwa unyofu huenda salama, bali apotoshaye njia zake atajulikana” Mithali 10:9
- Fedha sio lengo bali ni kifaa cha lengo
 - Fedha ni rasilimali unayotumia ili kutimiza lengo
 - Mungu atakupatia rasilimali unazohitaji kufanya kazi
- Uweza wa fedha dhidi ya watu umefafanuliwa na kuandikwa
 - Mara nyingi husababisha uamuzi usiofaa
 - Unaweza kufungwa jela
- Pesa zinaweza kuwa kama Mungu au sanamu ya kuabudiwa
“Hamwezi kumtumikia Mungu na mali” Mathayo 6:24
 - Kuzifuata pesa ni kumfuata Mungu asiye wa kweli
 - Unapokuwa mtumwa wa fedha unapoteza uhuru wako katika Kristo

2. Kutumia pesa kwa njia isiyofaa ni kumndanganya Mungu
 - Hazina zinazotolewa kanisani zimetolewa kwa Mungu
 - Kila kitu tulicho nacho ni chake, sisi tu mawakili tu
 - Mungu ana mpango kwa hazina zetu na jinsi tunavyo zitumia
 - Kutumia fedha kwa njia isiyofaa ni sawa na kuziiba
 - Unaliibia kanisa
 - Unamwiibia Mungu (*Malaki 3 :8*)
 - Kuiba hakudhihirishi upendo

“Pendo halimfanyii jirani neno baya” Warumi 13:10
3. Usimamizi mbaya ni utunzaji mbaya
 - Uwakili mbaya ni kutotumia fedha (rasilimali ya Mungu) inavyofaa
 - Kutumia vipawa vya Mungu vizuri kuzalisha matunda kwa ufalme
 - Kusimamia vipawa vya Mungu vizuri humtukuza Mungu
 - 4. Usimamizi bora wa fedha hujenga kuaminika
 - Kama huwezi kusimamia fedha
 - Huwezi kusimamia mambo ya kiroho

“Basi kama ninyi hamkuwa waaminifu kwa mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli” Luka 16:11
- Watu watakuamini ikiwa wewe unamwamini Mungu
“Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia”
Luka 16:10

II. Je kanuni za usimamizi wa fedha ni zipi

“Akawaambia, msitoe kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa. Msindhulumu mtu, wala msishitaki kwa uongo tena mtoshewe na mshahara wenu” Luka 3:13-14

1. Tosheka na kile Mungu amekutwalia
 - Muombe kwa kila unachohitaji
 - Mwamini Mungu kukutimizia mahitaji yako
2. Usitumie fedha kutimiza malengo fulani ambayo haukusudiwa
 - Usiitishie watu fedha kwa mradi mmoja kisha uzitumie kwa mwingine
 - Heshimu matoleo ya watu

3. Usitumie fedha za kanisa kwa mahitaji yako ya binafsi
 - Usiwahi kuchukua fedha za kanisa kutimiza mahitaji yako ya kibinafsi
 - Usiwape watu fedha za kanisa kwa mahitaji au matamaniao yao ya kibinafsi
4. Weka hesabu zote za fedha zilizopokewa
 - Rekodi pesa zote na zawadi unazopokea
 - Rekodi mahitaji yote ya pesa zinahitajika kila wakati
5. Wajibika kwa kila fedha ziliotumika
 - Weka rekodi za matumizi yote ya fedha
 - Weka risiti ya kila tumizi
6. Wekeza mpangilio wa gharama kubwa au ununuzi mkubwa wa bithaa.
 - Usiruhusu mtu mmoja katika uongozi kununua vitu vya hela nyingi
 - Dhibitisha hundi na vile hela zimetumika kwa ununuzi mkubwa
 - Pata cheti cha kuonyesha vile hela zimetumiwa
7. Mara kwa mara chapisha taarifa za kifedha
 - Pesa zilizopokelewa
 - Pesa zimetumika
 - Masalio
8. Husisha watu wasio husika katika huduma kukagua matumizi ya fedha za kanisa kwa muda fulani
 - Mtu kutoka inje anaweza kukagua nakala za fedha za kanisa
 - Fanya ukaguzi wa kifedha wa kila mwaka

III. Je, utajifunja vipi matumizi bora ya fedha?

1. Funza maadili ya Biblia kuhusu fungu la kumi (10%)

“Usiache kutoa zaka ya fungu la kumi katika maongeo yote ya mbegu zako,yatokayo shamba mwaka baada ya mwaka”Kumbukumbu la Torati 14:22

- Ongoza kwa mfano – toa fungu la kumi
 - Himiza utoaji wa mazao ya kwanza (**Methali 3:9**)
2. Onyesha nidhamu ya kifedha
 - Nakili matumizi yote ya fedha
 - Lipa madeni kwanza
 - Weka mikakati ya kukagua na kuchunguza fedha za kanisa

3. Mtumainie Mungu kukupa mahitaji yako

- Atakupa unachohitaji
- Mungu anawajali watu wake

“Walio matajiri waulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha”¹ Timotheo 6:17

4. Waruhusu waumini kujua fedha za kanisa

- Usifiche waumini mambo ya fedha
- Kuwa wazi na mwaminifu kwa utumizi na uhifadhi wa risiti.

IV. Ni faida zipi za usimamizi bora ya fedha?

1. Utajenga imani kwa waumini wako

- Waunini wakikuamini kwa fedha watakuamini kwa mambo mengine
- Watakuamini na hivyo basi kukufuata
- Watakuamini kutumia fedha kwa mambo makubwa

2. Utaepuka shida kubwa

- Majaribu ya Shetani hayatakusababisha kutenda jambo usingelifanya
- Tamaa haitakuvingia
- Utabaki mtakatifu na mfano mzuri kwa kondoo

3. Utajifunza kile nguvu za Mungu zaweza kutenda

- Utaona vile Mungu atajibia kila hitaji ulilonalo
 - Hii itakuza imani katika ahadi zake
 - Utajifunza kumtafuta Mungu kwanza
- “Basi utafuteni ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa”*
Mathayo 6:33

Zoezi La Kusimamia Fedha

Orodhesha mambo ambayo unaweza kufanya ili kuboresha usimamizi wako wa fedha

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____
6. _____
7. _____
8. _____
9. _____
10. _____

Sura ya Kumi na Moja

KUSIMAMIA MUDA

“...na moyo wa mwenye hekima hujua wakati na hukumu kwa maana kwa kila shauri kuna wakati na hukumu”

Mhubiri 8:5-6

Haijalishi ni taaluma ipi au kazi tutakayo ichagua ama kuifanya, sote tunajaribu kutimiza malengo mengi tukitumia rasilimali na muda tulio nao. Ingawaje rasilimali zinaweza kununuliwa au kutafutwa, muda ukishapita milele umepita, hauwezi kutumiwa tena wala kukombolewa. Kwa hiyo lazima tuwe waangalifu jinsi tunavyo utumia muda na tunautumia kufanya nini. Pia hatujui ni muda upi tulio nao kijumla kuutumia. Kwa maana hakuna anayejua ni lini Bwana utatuita nyumbani. Ni muhimu kuutumia muda tuliopewa kwa hekima. Vitabu vingi vimeandikwa kuhusu jinsi ya kusimamia muda, na tuna kusudia kukueleza kwa kifupi baadhi ya kanuni na mbinu utakazo tumia ili kutumia muda wako mwafaka. Katika sura hii tutatazama umuhimu wa usimamizi wa muda, jinsi ya kuutumia muda wako na hatimaye tutakupa vifaa vya kukuwezesha kutumia muda wako vizuri.

1. Umuhimu wa kupanga muda wako

1. Itakusaidia kutimiza kazi nyingi za huduma
 - Unaweza kazi ya huduma uliyokusudia
 - Hukusaidia kulenga kazi ya muhimu zaidi
 - Muda wako hutumika vizuri zaidi na kuleta matokeo bora

2. Hautapoteza muda

“Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima” Waefeso 5:15-16

- Hautatumia muda mwingi ukifanya mambo yasiyo muhimu
- Utaweza kutambua muda usio na matokeo bora
- Hautapoteza muda ukifikiria ufanye nini

3. Itakusaidia kutimiza malengo muhimu kwa muda unaofaa

- Husaidia kufahamu mambo yanayo takikana kufanya kwa muda unaofaa ili yasikupite
- Husaidia kukuelekeza taratibu kwenye lengo lako
- Shughuli zako zitapangwa kulingana na umuhimu wake

4. Husaidia kupunguza matatizo kazini

- Huondoa wasiwasi wa kutotimiza jambo muhimu
- Hukupa uwezo zaidi juu ya shughuli zako na ratiba
- Hukupa muda wa kustarehe na kupumzika
- Yote umwachie Mungu!

“Ukae kimya mbele za Bwana nawe umngojee kwa zaburi” – Zaburi 37:7

“Acheni mjue kuwa mimi ni Mungu– Zaburi 46:10

5. Hukuwezesha kupata muda wakati unapohitajika

- Hukusaidia kuyakabili matatizo ya muda
- Uhakikisha ya kuwa maswala muhimu yameshughulikiwa kwa muda unaofaa

II. Kanuni Za Usimamizi wa Muda

“Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikia pia“

1 Timotheo 4:15

1. Zipange shughuli zako kulingana na

- Umuhimu wake
- Kulingana na wakati zinapohitajika kukamilika
- Kulingana na majukumu uliyo nayo

2. Weka malengo maalum

- Wakati shughuli inatakikana kufanywa
- Muda utakao tengewa shughuli
- Atakaye husika na kazi

3. Shughuli zinazoweza kufanywa ka wakati mmoja ziwekwe pamoja

- Ziweke shughuli pamoja kuboresha utenda kazi
 - Kupiga simu, barua
 - Vipindi vya ushauri
 - Mahubiri na maandalizi ya mafunzo
 - Mikutano
- Usitoke kwa shughuli moja hadi nyingine
 - Utapoteza lengo
 - Unaweza kusahau yale ambayo tayari umekamilisha

- Hupoteza muda mwingi unapobadilisha majukumu
 - Muda mwingi hupotezwa unapotaka kulitekeleza jukumu moja hadi nyingine.
 - Ukiwa na mfumo unaotenda kazi, ni bora zaidi kuuendeleza
- 4. Yapange maamuzi yako kila siku
 - **Ahirisha** maamuzi yanayoweza kufanywa baadaye
 - **Kasimu** maswala kwa wataalamu ambao wanaweza kuyatekeleza vyema
 - **Amua** maswala yanayohitaji uamuzi wako
- 5. Badilisha ratiba yako ya kila siku kulingana na mahitaji yako
 - Usiwe na ratiba ambayo haikupi muda wa ziada na badala yake inautumia muda wako wote
 - Tarajia yasiyo tarajiwa yanaweza kuibuka na kuharibu ratiba yako
 - Kuwa na kipindi cha mapumziko na wakati wa kula
 - Mpe Mungu nafasi ya kubadilisha ratiba yako
 - Kupitia nafasi mpya ya huduma
 - Kupitia mtazamo mpya
- 6. Kabiliana haraka na usumbufu
 - Usitatie jambo ambalo lingetanguliwa baada\
 - Isikize shida ile na kisha uamue kama utacheleweshwa ishughulikiwe au fanya uamuzi
 - Kama unaweza kufanya uamuzi wa haraka, ufanye kisha uendele

III. Jinsi ya kuusimamia muda wako

1. Ipange siku yako
 - Uwe na orodha ya mambo unayohitaji kufanya
 - Tambua kile kinatakikana kukamilishwa leo
 - Tambua kinachotakiwa kufanywa leo
 - Tambua linalotakikana kuamuliwa leo
 - Tambua jambo lingine ambalo ungependa kufanya leo kama muda utapatikana
 - Uwe na malengo yaliyoimarishwa vizuri
 - Fahamu la muhimu zaidi
 - Elewa malengo unayo
 - Fanya maswala ya muhimu kwanza
 - **Panga likozo fupi** – mwili wako na mawazo yako vinahitaji kupumzika mara kwa mara
 - Chagua wakati ambao unakufaa vizuri na ufanye vitu vya maana wakati huo
 - Usifanye maamuzi mazito jioni wakati umechoka
 - Panga shughuli ambazo sio za muhimu wakati umechoka baada ya chakula cha mchana e.t.c)

2. Kuwa Stadi
 - Piga simu zote kwa wakati mmoja
 - Kuwa na muda wako wa kusoma na kutengeneza mahubiri
 - Jaribu kuepuka migogoro na mambo yasiyo ya maana
 - Fanya mambo ambayo yanatakikana kufanywa leo
3. Usitumie muda kusimamia mambo ambayo wengine wanaweza kuyafanya
 - Gawa kazi kwa viongozi wengine ikiwezekana
 - Usifanye kazi ambazo wengine wanaweza kufanya
 - Kuna msembo wa zamani - *“Msaidie mtu, na atakuwa jukumu lako”*
(k.m vitu vidogo ambavyo unawafanyia wengine inaweza kuwa tabia ya kila siku ama tabia ambazo ni ngumu kuwacha.)
4. Simamia mikutano yenye matokeo
 - Kuwa na muda wa maombi wa kukuongoza
 - Andaa ajenda kila mara
 - Zuia kujadili mambo ambayo hayako kwenye ajenda
 - Kwa sababu watu hawako tayari kujadili swala
 - Kwa sababu mara kwa mara hayako katika ajenda
 - Kazia ajenda na wakati
 - Jadili tu mapendekezo yanayoweza kuamuliwa
 - Usiwe na majadiliano isipokuwa ukitaka kutafuta habari
 - Itasaidia mkutano kukazia maswala la mswada
 - Itawezesha majadiliano kufikia uamuzi
 - Gawa majukumu
 - Inajenga ushirikiano na umoja
 - Inafanya kila mtu mkutani awajibike
 - Andika majadiliano, maamuzi na makubaliano kupitia kumbukumbu za mikutano
 - Andika mambo yaliyo jadiliwa
 - Andika yote ambayo yaliamuliwa
 - Andika majukumu watu walitengewa

IV. Vifaa viwili vya usimamizi wa muda

1. Tengeneza fomu ya wakati (ama tumia kalenda ya kila siku ama ya mwezi)
 - Itumie kupanga wakati katikati ya wiki ama mikutano iliyopangwa
 - Inakusaidia kukagua vile muda wako unatumika
 - Inaweza ikatumiwa kupanga kazi zako za kati ya wiki
2. Tengeneza ratiba ya shughuli
 - Itakusaidia kupanga siku yako, wiki na hata mwezi
 - Itakuwezesha kufanya kazi muhimu za huduma kwanza
 - Inasaidia kutosahau shughuli na mikutano muhimu

ZOEZI

Sampuli ya kusimamia muda wako

Tumia ratiba iliyochorwa hapa na uonyeshe siku za kupumzika, somo la Biblia, mtayarishaji wa ujube, ibada ya wiki ijayo n.k zilizobaki unaweza kuzijaza kulingana na mahitaji yako.

	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi	Jumapili
8.00am							
8.30							
9.00							
10.00							
10.30							
11.00							
11.30							
12.00pm							
12.30							
1.00							
1.30							
2.00							
2.30							
3.00							
3.30							
4.00							
4.30							
5.00							
5.30							
6.00							
6.30							
7.00							
7.30							
8.00							
8.30							
9.00							
9.30							

MFANO

	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi	Jumapili
8.00am		Kupiga simu		Kusoma Bibilia		familia	
8.30		Kupiga simu		Kusoma Bibilia		familia	
9.00		Offisini		Kusoma Bibilia	Ushauri	familia	kusifu
10.00		Offisini		Kusoma Bibilia	Ushauri	familia	kusifu
1030		Offisini			Ushauri	familia	kusifu
10.30		Offisini			Ushauri	familia	kusifu
11.00							kusifu
11.30							kusifu
12.00pm	Chakula	Chakula	Chakula	Chakula	Chakula		Chakula
12.30	chakula	Chakula	chakula	Chakula	chakula		Chakula
1.00							
1.30							
2.00			Kuandaa ujumbe				
2.30			Kuandaa ujumbe				
3.00			Kuandaa ujumbe				
3.30			Kuandaa ujumbe				
4.00							
4.30							
5.00	kinyuaji	Kinyuaji	kinyuaji	Kinyuaji	kinyuaji		
5.30	kinyuaji	Kinyuaji	kinyuaji	Kinyuaji	kinyuaji		
6.00							
6.30							
7.00		Mkutano				Kujiandaa kwa ibada	
7.30		Mkutano				Kujiandaa kwa ibada	
8.00		Mkutano				Kujiandaa kwa ibada	
8.30						Kujiandaa kwa ibada	
9.00							
9.30							

Sura ya Kumi na Mbili

KUSIMAMIA HABARI

Watu wenye akili huweka akiba ya maarifa...

Methali 10:14

Moja ya rasilimali iliyopuuzwa mno kanisani ni habari. Habari hii labda inawahusu washirika wa kanisa au habari kuhusu huduma nyingine kanisani, shughuli au rasilimali zilizopo. Habari hii ni utajiri mkubwa, unaotusaidia kufanya huduma tuliyoitiwa na kwa hivyo ni muhimu kufahamu habari zilipo na jinsi ya kuzifikia. Habari lazima zikusanywe na kuhifadhiwa na kanisa, haswa habari kuhusu washirika pamoja na shughuli au vipawa walivyokirimiwa. Habari nyinginezo sasa zinapatikana kwa mtandao, maktaba au maduka yanayouza vitabu. Ili kupokea habari tunavyohitaji kwa wakati unaofaa, lazima tuwe na habari hiyo ama tujue tutakapo ipata. Hali hii ndiyo usimamizi wa muda. Tarakilishi husaidia mno, lakini sio lazima uwe na tarakilishi ili uhifadhi habari. Unaweza kutumia njia nyinginezo, ambazo pia zinafanya kazi. Katika surah hii tutatazama umuhimu wa usimamizi wa habari na jinsi ya kukusanya na kuhifadhi habari kwa matumizi ya siku za usoni.

I. Umuhimu wa Usimamizi wa habari

« Kila aliye na busara hutenda kazi kwa maarifa » - Methali 13:16

1. Huongeza ufahamu wako kuhusu rasilimali ulizo nazo
 - Habari za washirika wako, kuhusu karama za kiroho na ujuzi
 - Habari juu ya rasilimali nyingine za kanisa (vitabu, kanda za video, mafundisho ya Biblia n.k)
 - Habari kuhusu shughuli za kanisa na huduma (nani, nini na wapi)
2. Itakuepusha kupoteza muda ukitafuta habari
 - Hautatumia muda mwingi kuzitafuta stakabadhi.
 - Utajua kumwendea nani kwa mahitaji maalumu
 - Sio lazima uwatafute watu ili wakupe habari unayohitaji
3. Itakusaidia kufanya maamuzi bora
 - Maamuzi huwa mazuri kulingana na habari zilizotegemewa
 - Kuwa na habari zinazohitajika ni jambo la muhimu
 - Kufahamu ni bora kuliko kudhania
4. Ni muhimu kwa upangaji mwema
 - Mpango huwa mzuri kulingana na habari zilizotegemewa
 - Habari mbaya huleta matokeo mabaya
 - Huwezi kupanga kuhusu kitu usichokijua

5. Inakuwezesha kuona fursa katika huduma
 - Kujua ulicho nacho kitakuwezesha kuwa mbunifu
 - Hukuwezesha kufuatilia uwezekano wa huduma
 - Kulingana na ufahamu wa washirika na vipawa vyao
 - Kulingana na ufahamu wa jumua

II. Kanuni za Kusimamia Habari

“Enenda na wenye hekima nawe utakuwa na hekima” Methali 13:20

1. Kusanya na uhifadhi habari unazohitaji tu
 - Habari zinazohitajika kwa kufanya uamuzi
 - Habari zinazohitajika ili kuliendeza kanisa
 - Habari zitakazo wawezesha waumini kufahamu wajibu wao kanisani
2. Imarisha habari baada ya muda
 - Habari hubadilika haraka na hata kupitwa na wakati
 - Imarisha njia mwafaka za kupokea habari
 - Orodha ya wanaohudhuria darasa
 - Habari kuwahuu washirika wapya kanisani
 - Watumie viongozi wa kanisa kukusanya habari
 - Wahusika wa huduma
 - Matokeo ya huduma, shughuli
 - Chunguza fomu ya washirika kila mwaka
 - Kubadilisha anwani
 - Nambari mpya za simu na barua pepe
3. Kusanya na uhifadhi habari za shughuli za kanisa
 - Usitangaze wala kuchapisha habari za mtu binafsi bila ya idhini yake
 - Hifadhi habari hii kwenye kabati linalofungwa
 - Zingatia uaminifu / usiri
4. Tengeneza mfumo wa kupanga na kuweka habari maalum
 - Kwa utenda kazi (mada, lengo, matumizi)
 - Kulingana na huduma
 - Kulingana na jina la mshirika

5. Kuwa na mpango wa kuitumia habari
 - Usikusanye habari bila ya kuwa na mpango wa kutumia
 - Fahamu kusudi la kila habari iliyokusanywa
 - Kama huna haja nayo usikusanye wala kuhifadhi
6. Simamia habari
 - Usidhanie kwamba habari imekusanywa au kuhifadhiwa
 - Iwe sambamba na wakati
 - Rekebisha / Chunguza habari zako mara kwa mara

III. Jinsi ya kusimamia habari

1. Amua habari unayohitaji
 - Washirika wa kanisa
 - Shughuli za kanisa
 - Rasilimali za kanisa (Vitabu, vyumba, vifaa na kadhalika)
 - Rasilima za jumua (hotel, jumba za mikutano, na wachuuzi)
2. Kusanya na uhifadhi habari kuhusu washirika wa kanisa
 - Majina yao, anwani, nambari za simu, barua pepe
 - Karama zao za kiroho
 - Uzoefu na ujuzi wao
 - Shughuli zao kanisani na wanao husiana nazo
3. Kusanya na uhifadhi habari kuhusiana na shughuli zao kanisani
 - Wanavyohudhuria ibada
 - Wanavyohudhuria darasa lakuji funza Bibilia
 - Wanavyohudhuria katika vikundi vidogo
4. Kuwa na mipango maalum wa kupanga na kupata habari maalum
 - Mahali habari zinapohifadhiwa (Tarakilishi, faili)
 - Eneo ya manufaa katika mtandao
 - Nani aliye na habari
5. Kuwa na mpango wa kutumia habari
 - Ujumbe upi utakusanywa
 - Lengo la kila habari
 - Nani aliye na jukumu la kukusanya habari
6. Mpe mtu jukumu la kusimamia habari
 - Hali ya kukusanya habari iendeleo
 - Kuwa na mahali pa kuhifadhi ujumbe
 - Wezesha upangaji na usimamizi bora

